# Nipashe

Jumanne Agosti 4, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580301

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710




## Makonda akabidhi ofisi Dar na kuomba msamaha

UKURASA 3




UKURASA 11

# Kilio cha uhaba mafuta kila kona

**WATUMIAJI** waenda vituoni na kuambulia patupu, wamiliki wapandisha bei kinyemela, EWURA kutoa taarifa rasmi leo...*Endelea ukurasa wa 2*




Madereva wa vyombo vya moto, wakiwa katika foleni kubwa ya kununua mafuta mjini Mpanda, mkoani Katavi jana, kutokana na uhaba mkubwa wa bidhaa hiyo. **PICHA: NEEMA HUSSEIN**

## BILIONEA LAIZER AIBUA TENA JIWE LA BIL. 4.8/-

UKURASA 3

## Lissu, Nyalandu, Majinge wapenya urais CHADEMA

UKURASA 2



Tundu Lissu



Dk. Maryrose Majinge



Lazaro Nyalandu




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play · App Store



**MICHEZO** SIMBA YATIKISA DAR, CHAMA AKOGA NOTI UK.24

MAONI, KATUNI UK.6



Naibu Mkurugenzi wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA-JKT) anayeshughulikia Utawala, Kanali Absolomoni Shausi, akikata utepe kuzindua magari na pikipiki zilizonunuliwa na kampuni zake za SUMA-JKT Guard na ya Usafi na Unyunyiziaji Dawa, katika hafla iliyofanyika jijini Dar es Salaam jana. Kushoto kwake ni Mkurugenzi Mwendeshaji wa kampuni hiyo, Luteni Kanali, Joseph Masanja. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Kilio uhaba wa mafuta kila kona

**Na Waandishi Wetu**

UHABA wa mafuta ya petroli na dizeli, umeyakumba maeneo mbalimbali nchini na kusababisha watumiaji wa vyombo vya usafiri kuzunguka vituo mbalimbali na kuambulia patupu huku baadhi ya maeneo wakikaa kwenye foleni ndefu.

Pamoja na uhaba huo, bei ya mafuta imepanda kimya kimya tofauti na bei elekezi iliyotangazwa mwanzoni mwa mwezi uliopita hadi kufikia Sh. 1,837 kwa lita ya petroli, huku Mamlaka ya Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA), ikifafanua kuwa bei ilipanda kupusha uhaba na kulazimika kuruhusu shehena iliyokuwepo iliyoingizwa kwa bei ya juu kuuzwa kwa bei ya soko.

Aidha, katika eneo la Tabata baadhi ya vituo havijauza huduma hiyo kwa takribani wiki moja sasa, hali inayowasumbua watumiaji na kushindwa la kufanya. Hatua hiyo imesababisha baadhi ya madereva kuegesha vyombo vyao vya moto kwa muda wakisubiri hali hiyo kutengemaa.

Katika eneo la Tabata vituo vingi havikuwa na bidhaa hiyo kiasi cha kuwalazimu kuhama kutoka kituo kimoja kwenda kingine na bado hawakufanikiwa, huku waathirika wakuu wakiwa ni waendesha bodaboda na bajaji.

"Nimetembea kwenye vituo vitatu hadi sasa. Sheli (vituo vya mafuta vya Camel na Lake Oil Sanene na Oilcom segerea hakuna mafuta. Wafanyakazi wapo lakini wanasema hakuna mafuta. kama unavyoona pikipiki yangu ina mafuta kidogo, kuliko niyamalize kwa kutafuta mafuta bora haya machache yahifadhi nipakie wateja," alisema Shaibu Hussein.

Naye mmiliki wa gari dogo aliyekutwa kwenye kituo cha mafuta eneo la Tabata, Jane Mushi alisema alianza kutafuta huduma hiyo juzi jioni lakini kila alikokwenda hakuwapo na wafanyakazi wa vituo hivyo walidai kuwa hawajapata mafuta kutoka kwa wasambazaji wakubwa.

Katika eneo la Kigamboni, madereva walionekana wakihaha kwa takribani siku tatu kutafuta bidhaa hiyo kiasi cha wengine kuegesha vyombo vya usafiri na wengine wakiomba kupunguziwa mafuta kutoka kwenye magari mengine ili kufikisha vyombo vyao nyumbani.

**KATAVI**

Mjini Mpanda, jana hali ilikuwa ngumu kiasi cha kutokea vurugu zilizovilazimu vyombo vya ulinzi na usalama kuingilia kati na kuwalazimisha wananchi kukaa kwenye mistari ili kupata huduma hiyo.

Nipashe ilishuhudia wananchi wakiwa kwenye misururu mirefu hasa wenye pikipiki na bajaji na wengi wakiamua kuegesha vyombo hivyo kutokana na kukosa huduma hiyo.

Kwa takribani siku tatu vituo vingi katika mji huo havina mafuta ya petroli isipokuwa kimoja ambacho kilifurika wanaohitaji huduma hiyo.

**ARUSHA**

Mkoani Arusha, tangu juzi hakuna huduma hiyo ndani ya jiji la Arusha, huku vituo vya barabarani kutoka Arusha mjini hadi Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA).

"Tangu juzi hakuna mafuta kwenye vituo vya mafuta, mara kadhaa nimekwenda huduma wanasema hakuna mafuta, mfana jana nilikuwa naelekea KIA katika vituo vyote vya barabarani hakukua na mafuta," alisema.

**KAHAMA**

Wilayani Kahama mkoani Shinyanga, huduma za usafiri ziliathiriwa kutokana na kukosekana kwa mafuta kwa takribani wiki moja hali iliyowalazimu baadhi kuviegesha.

Amos Ben, dereva wa pikipiki katika kituo cha mabasi mjini Kahama, alisema alikwenda kwenye vituo vingi lakini vimefungwa kwa kuwa hakuna mafuta hali iliyowafanya kutafuta kwa muda mrefu.

**EWURA YANENA**

Alipoulizwa na Nipashe kwa ujumbe mfupi wa maandishi, Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa Mamlaka ya Udhibiti ya Huduma za Nishati na Maji (EWURA), Titus Kaguo, alithibitisha uhaba huo lakini akasema jambo hilo linakuzwa.

"Ni kweli kuna uhaba lakini watu wana-exagrate (wanakuza)," alisema.

Akizungumza na Nipashe kwa simu, Kaguo alifafanua wakati wa Corona matumizi ya mafuta yalishuka kwa asilimia 17, lakini baada ya shughuli kurejea yalipanda huku kukiwa hakuna shehena mpya.

"Tuliagiza mafuta mengine lakini meli ilikwama baharini kutokanana upepo wa monsoon, badala ya kufika Julai 27, imefika juzi. Hakuna mgomo wa wafanyabiashara ila shehena iliyokuwepo ilikwisha kutokana na mahitaji makubwa,"alifafanua Kaguo.

Aidha, alisema mahitaji ya mafuta yaliongezeka kutoka lita milioni 2.5 kwa siku hadi milioni 4.5 baada ya shughuli kurejea na kwamba uhaba uko kwenye Petroli kutokana na kuwa na watumiaji wengi.

Kuhusu bei kupanda hivi karibuni, alisema baada ya kuona kuna uhaba na ndani ya siku tatu hakutakuwa na petroli, EWURA iliridhia shehena iliyokuwepo iliyoagizwa kwa bei ya juu kipindi cha nyuma kuuzwa kwa bei ya soko wakati huona ndiyo sababu ya bei kupanda kwa muda mfupi.

Kaguo aliwatoa hofu watanzania kuwa hakuna uhaba mkubwa kiasi hicho kwa kuwa kuna meli tatu zimfika na kwamba watu anakuza huku akitoea mfano eneo la Kigamboni lenye vituo 14 na vitatu pekee havina Petrol na kwamba kusema hakuna mafuta ni kupotosha.

Juni 29, mwaka huu, EWURA ilisema maghala ya mafuta yana lita 92,435,539 za petroli ambazo zingetosheleza kwa siku 25 na Deseli walikuwa na lita 147,398,593 zilizotosheleza kwa siku 29.

Mamlaka hiyo ilisema ina shehena ya petroli yenye tani 39,772 iliyotegemewa kuwasili nchini Julai Mosi, mwaka huu.

Bei ya mafuta mafuta hayo ilipomoka kutoka zaidi ya Sh.2,000 kwa lita ya Petroli, kufikia Sh. 1,520 na Disel 1,546 kwa jiji la Dar es Saalam.

Pia Juni 30, mwaka huu, mamlaka hiyo ilitagaza tena bei mpya ambayo ilikuwa na ongezeko la kati ya Sh.170 hadi 173 kwa Petroli na Disel, na kufikia Sh. 1,520 hadi 1,693 kwa jiji la Dar es Salaam.

Kila Jumatano ya mwanzo wa mwezi, EWURA hutoa bei elekezi ya mafuta ya petrol, na dizeli na mafuta ya taa kulingana bandari inayohudumia eneo husika. Bandari hizo ni Mtwara, Tanga na Dar es Salaam.

***Imeandikwa na Salome Kitomari (DAR), Shaban Njia (KAHAMA), Neema Hussein (KATAVI) na Allan Isack (ARUSHA)***

## Lissu, Nyalandu, Majinge wapenya urais CHADEMA

**Na Mary Geofrey**

KAMATI Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), imepitisha majina matatu ya watiania wa urais kupitia chama hicho.

Waliopitishwa ni Dk. Mayrose Majinge, Lazaro Nyalandu na Tundu Lissu, kati ya wagombea saba waliotia nia ambao Mkutano Mkuu wa Baraza Kuu la CHADEMA uliyapigia kura na kupata mgombea mmoja.

Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alitangaza majina ya watiania waliopitishwa jana jijini Dar es Salaam, mbele ya wajumbe wa Mkutano wa Baraza Kuu la chama hicho.

Alisema jina moja lililopitishwa na Mkutano huo Mkuu wa Baraza Kuu, litapitishwa na Mkutano Mkuu wa CHADEMA utakaofanyika leo.

Wagombea hao watatu walipata fursa ya kujinadi na kujieleza mbele ya mkutano huo na kuulizwa maswali na wajumbe kabla ya kuwapigia kura.

**MBOWE AELEZA ALIVYOACHA KUTIA NIA**

Kwa upande wake, Mbowe alieleza sababu za kutotangaza nia ya kuwania kinyang'anyiro hicho, licha ya kuchukuliwa fomu na baadhi ya wanachama.

Katika mchakato huo, wanachama 11 walichukua fomu ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa na chama hicho akiwamo Mbowe, lakini ni wanachama saba tu ndio waliorudisha na kutangaza nia.

Mbowe alisema alikacha mbio za kugombea urais wa Tanzania ili akijenge chama hicho.

Alisema tamaa zake haziwezi kuwa na thamani, ikilinganishwa na thamani ya CHADEMA.

"Nilifuatwa nikaambiwa mwenyekiti gombea urais, nikakubali, lakini sikutangaza nia. Hofu ikaibuka mwenyekiti anagombea, makamu anagombea, nikasoma kwenye mitandao, lakini mimi binafsi kama Mbowe hiki chama kwangu ni kama mtoto, haiwezekani tamaa zangu binafsi zikawa za maana kuliko uhai wa chama chetu," alisema.

Mbowe alisema hatoiacha safari ya kuijenga CHADEMA kwa sababu ya maslahi yake binafsi. "Tumeamua sana kuijenga CHADEMA, hatutaiacha safari hiyo kwa sababau ya maslahi binafsi," alisisitiza Mbowe.

Kadhalika, Mbowe aliwataka wajumbe kuchagua mgombea anayefaa na kuepuka mipasuko.

"Nguvu yetu ni umoja wetu, tutoke hapa wote tuna nyuso za furaha, tumpate mgombea katika mazingira ya kuujenga umoja wetu na siyo mpasuko kati yetu," alisema.

Mbowe pia aliwasihi wajumbe wa baraza hilo kutowabagua WanaCHADEMA waliowahi kuwa wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Tunahitaji kuonyesha upendo ndani ya chama chetu kuimarisha Tanzania kujenga umoja wetu, hatuhitaji kufanya makosa ya CCM kutubagua na sisi tukafanya ubaguzi dhidi ya wanachama wenzetu kwa sababu walikuwa CCM, tunahitaji umoja wa kitaifa, tunahitaji mtu mmoja," alisema.

**USHIRIKIANO NA ACT-WAZALENDO**

Kadhalika, Mbowe alisema CHADEMA inaendelea kufanya mazungumzo na Chama cha ACT-Wazalendo, kwa ajili ya kuunda nguvu moja ili kuing'oa CCM madarakani.

Alisema CHADEMA na ACT-Wazalendo kwa sasa vinapanga mashambulizi ya kisiasa dhidi ya CCM.

"Hatutaingia kwenye ushirikiano kama fasheni, tutaingia kwenye ushirikiano kama kuna watu wako makini, ambao hawatatuuza njiani, tunakubaliana jamani?" Alihoji Mbowe huku akishangiliwa.

Aliendelea: "Tunaendelea na mazungumzo, lakini niseme bayana, katika mazungumzo tunayoendelea nayo, tunaendelea na mazungumzo na Chama cha ACT-Wazalendo."

Alisema kuhusu mategemeo ya maongezi yao inatategemea mawazo ya kila mmoja, na kwamba pia watazungumzia kuachiana nafasi ya urais Zanzibar. Mbowe alisema katika mazungumzo hayo, CHADEMA iko tayari kuachia nafasi za kugombea.

"Huko nyuma tuliingia kwenye mazungumzo ya ushirikiano wa vyama vingine, miongoni mwa sababu ni unyonge wa chama chetu katika baadhi ya maeneo, lakini leo tunashirikiana na vyama vingine kwa sababu kuna maeneo vyama vingine vina nguvu kuliko wagombea wetu," alisema Mbowe.

Kwa mujibu wa Mbowe, CHADEMA kinaweza kuwa chama kikubwa, lakini kinapaswa kuheshimu mawazo ya chama kingine ambacho kinataka kushirikiana nacho.

"Tumheshimu kila mwenzetu kwa ukubwa wake, ukubwa wetu utujengee unyenyekevu usitujengee kiburi, tunapoona kuna sababu ya kushirikiana, tutashirikiana na tukiona hakuna maslahi mapana ya chama na taifa letu, tutafikiria tofauti," alisema Mbowe.

Katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, vyama vya upinzani viliunda ushirikiano uliounda umoja uliotokana wakati wa Bunge la Katiba na kuitwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (UKAWA) na kumsimamisha Waziri Mkuu mstaafu, Edward Lowassa, aliyechuana na Rais John Magufuli.

## HABARI KITAIFA




Bilionea Saniniu Laizer (mwenye vazi kimasai), akiwa ameshika mfano wa hundi ya zaidi ya Sh. bilioni 4.8 baada ya kuiuzia serikali jiwe la tatu la madini ya Tanzanite lenye kilo 6.33 na kukabidhiwa fedha hizo na Waziri wa Madini, Doto Biteko (wa tatu kushoto), huko Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Laizer aibuka na jiwe la bil. 4.86/-

**Na Cynthia Mwilolezi, SIMANJIRO**

NI Laizer tena! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya Bilionea Saniniu Laizer kupata tena jiwe lingine la tanzanite lenye uzito wa kilogramu 6.33 ambalo serikali imelinunua kwa Sh. bilioni 4.86.

Juni 23, mwaka huu, Laizer alipata mawe makubwa mawili yenye thamani ya Sh. bilioni 7.8, ambayo aliyauza kwa serikali na kisha kupelekwa kuhifadhiwa kwenye Makumbusho ya Taifa.

Jana, Waziri wa Madini, Dotto Biteko, akizungumza katika eneo la Mirerani yaliko machimbo ya tanzanite wakati Laizer akikabidhiwa hundi ya Sh. bilioni 4.86, alisema jiwe hilo pia litahifadhiwa kwa ajili ya kuanzisha utalii wa madini.

"Tunawapenda Watanzania wanaochimba kwa haki na hawatadhulumiwa, na kila atakayepata jiwe lake atapata stahiki yake. Serikali tunataka tuanzishe utalii wa madini nchini, na ndiyo maana leo tumenunua jiwe hili lililopatikana Juni 29 mwaka huu na tulipata taarifa siku hiyo hiyo.

"Lengo letu kubwa ni kuongeza thamani ya madini hayo nchini na kuachana na kunufaisha nchi zingine kwa malighafi," Bitoke alisema. Kwa mujibu wa waziri huyo, kupitia ununuzi huo, serikali imepata mrabaha wa Sh. milioni 293, jambo ambalo linaipa nguvu ya kuongeza maeneo ya uthaminishaji madini.

Aliwataka Watanzania na wachimbaji kupuuza wanaolidanganya taifa kuwa serikali inamdhulumu Bilionea Laizer, kwa kuwa kabla ya ununuzi huo, wametumia wathaminishaji watatu kufanya tathmini ili kumlipa stahiki yake.

Kuhusu wanaoendelea kutorosha madini kwenda nje ya nchi, Biteko alionya kuwa hakuna mfanyabiashara atakayetoboa au kufanikiwa kutekeleza dhamira hiyo.

"Vyema mkajua pale mnapokuwa watatu au wawili, mkapanga njama zenu mjue mmoja wenu atatupa taarifa zenu zote. Na mnapopumua, mjue na sisi serikali tunafahamu mbinu zenu mpya zote mlizobuni.

"Serikali ina fedha nyingi na itaendelea kununua madini yenye uzito mkubwa ili dunia ije Tanzania kutalii na kuongeza mapato yetu.

"Katika hili, kila siku ninapata simu za nje ya nchi, wakiomba kununua mawe haya tulionunua kwa Bilionea Laizer na mimi ninawajibu kwa kiburi 'tuna fedha tunanunua wenyewe', maana tumechoka kuzalisha malighafi za nchi zingine," alisema.

Waziri huyo pia aliwataka wachimbaji wadogo kuendelea kusubiri utaratibu unaowekwa na serikali kuhusu uchimbaji kwenye Kitalu C ambacho ubia kati ya serikali na mwekezaji umevunjika.

Waziri Biteko alionya uvamizi huo akisema: "Msivamie pale panalindwa, na atakayeingia hapo hakuna atakayemsaidia. Msiwe na wasiwasi, kwa sababu hatuna mpango wa kuwapa wawekezaji tena, maana kwa miaka mingi walipokuwapo hatujawahi pata jiwe la uzito wa kilogramu tisa, saba, wala tatu.

"Ni bora tuendelee kuwaongezea ujuzi wachimbaji wadogo, ambao sasa wameonyesha maajabu na Tanzania kuongoza duniani, kwa kuwa na mawe yenye uzito mkubwa."

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Phillip Mpango, aliwataka wananchi kuwa wazalendo, ili madini hayo yanufaishe wote na ili kulinda rasilimali hizo vema kila mmoja akatumia haki yake ya kupiga kura kwa kuchagua viongozi watakaoendeleza sekta hiyo na kupageuza Mirerani kuwa sehemu ya maajabu.

Mkuu wa Majeshi nchini, Jenerali Venance Mabeyo, alisema vyombo vya ulinzi na usalama vitaendelea kulinda rasilimali za nchi ili kila mmoja anufaike nazo.

Bilionea Laizer alishukuru serikali kwa kununua madini hayo na kuwaomba wachimbaji wenzake kuendelea kuwa wazalendo, ili kuinua uchumi wa taifa.

"Wale wanaosema nimedanganywa, hapana wala sijadanganywa wala kuibiwa, ni waongo. Serikali imenipa stahiki yangu na kweli serikali hii haina mfano kwani imewaleta maendeleo makubwa yakiwamo maji kwenye vijiji vya umasaini ambako walikuwa wakitumia punda kutafuta maji umbali mrefu, sasa tumeachana nao," alisema.

# Makonda akabidhi ofisi na kuomba msamaha

**Na Joseph Mwendapole**

ALIYEKUWA Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda, amekabidhi ofisi kwa Mkuu wa Mkoa mpya, Aboubakary Kunenge na kuwaomba msamaha kwa kazi wake huku akiwataka wamwache akapumzike kwa amani na kumlea mtoto wake.

Hafla ya makabidhiano ilipangwa kufanyika saa 3:00 asubuhi lakini Makonda aliingia kwenye ofisi hiyo saa 5:15 na kulakiwa na kundi kubwa la wapigapicha na waandishi wa habari.

Waandishi hao ambao walifika mapema kwenye ofisi hiyo majira ya saa 2:30 asubuhi, walianza kumpiga picha tangu anashuka kwenye gari lake nje ya ofisi hizo hadi anaingia ofisini.

Baada ya kuingia, waandishi wa habari waliarifiwa na maofisa wa ofisi hiyo kuwa Makonda ana mazungumzo na Mkuu wa Mkoa yatakayochukua dakika 20 na ndipo wataruhusiwa kuingia.

Alipoanza kuzungumza, Makonda alisema hatasahau vita vitatu ambavyo alipigana na kusababisha watu kupiga kelele ikiwamo ya kupambana na mapapa wauzaji na wateja wa dawa za kulevya.

Makonda alisema anawapenda wakazi wa Dar es Salaam kwa kuwa amewatumikia kwa uaminifu na siku zote alikuwa akimwomba Mungu amsaidie asifanye baya ambalo ataulizwa mbinguni.

"Ninaamini nimetumia uwezo wangu wote akili zangu zote na vipaji vyangu vyote hatimaye naamini mwendo nimeumaliza salama. Kama binadamu inawezekana nina mapungufu (upungufu) yangu mnisamehe pale nilipoenda kinyume cha mapenzi yenu," alisema.

Makonda alisema Julai 15, aliamua mwenyewe kuondoka na kwenda kwenye majukumu mengine baada ya kuacha alama kwa wakazi wa Dar es Salaam kwa kazi kubwa aliyofanya.

Alisema pamoja na kelele za watu, Rais John Magufuli aliendelea kumwamini na kumpa moyo hali iliyosababisha kuendelea kupambana na watu hao na hatimaye kushinda mapambano.

Pia alisema atamuenzi Rais Magufuli kwa vitendo kwa kuwa ni mtu wa mfano kwake na atakayejaribu kumsema vibaya, atasimama kupambana naye hata kama hayuko kwenye nafasi yoyote.

Makonda aliwashukuru waliokuwa wasaidizi wake wakiwamo wafagizi ambao alisema wasingekuwa wema wangeweza hata kutumiwa na watu wabaya kumwekea sumu kutokana na watu aliokuwa akipambana nao.

"Nawashukuru wote tuliofanya kazi pamoja kwa sababu vita nilizopambana ningeweza kupewa sumu lakini wamekuwa waaminifu na nimeondoka ofisini nikiwa na furaha,"

Alisema anamshukuru mke wake kwa kuwa mvumilivu kwa maneno ya kashfa na kejeli dhidi yake kwa miaka yote ya utumishi wake kwenye nafasi hiyo na kwamba ataendelea kusimamia imani yake bila kujali maneno ya ovyo anayohusishwa nayo.

"Mke wangu aliniambia kuwa mbona kuna maneno mengi huku instagram kuhusu wewe nilidhani watu watakuacha baada ya kuacha kazi mbona wanakufuatilia nikamwabia waache waseme ukiona husemwi jua huna la maana. Nilimwambia kusema kwangu ndio mtaji wangu na huwezi kusemwa kama huna la maana," alisema Makonda

Makonda alimshukuru Rais Magufuli kwa kumteua Kunenge kuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam kwani ni mchapakazi ambaye atayaendeleza yale yote mazuri waliyokuwa wakiyafanya pamoja.

Hata hivyo, alimtaka mkuu

Ujamaa Community Resource Team
EMPOWERMENT JUSTICE STEWARDSHIP
**PO Box 15111, Arusha, Tanzania**
**www.ujamaa-crt.org**

115842202

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MIRADI.**

SHIRIKA LA UJAMAA COMMUNITY RESOURCE TEAM NI SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI LINALOJISHUGHULISHA NA KUJENGA UWEZO WA JAMII KATIKA MASUALA YA UTAWALA BORA, ARDHI NA MAZINGIRA KATIKA MIKOA YA ARUSHA NA MANYARA.

SHIRIKA LINAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA LITATEKELEZA MIRADI MIPYA IPATAYO MITANO KAMA INAVYOAINISHWA HAPA CHINI KUANZIA AUGUST 2020 MPAKA 2021

1. UCRT KWA KUSHIRIKIANA NA CARBON TANZANIA (CT) KUPITIA UFADHILI WA THE NATURE CONSERVANCE (TNC) ITATEKELEZA MRADI WA HEWA UKAA (CARBON MARKET) AU REDDs KATIKA VIJIJI VYA YAEDA CHINI, MONGO WA MONO, ESHKESH, DOMANGA NA ENDANYAWISH, ENDAMAGHA, MIKOCHENI, QANG`DED, MBUGA NYEKUNDU, JOBAJ, DUMBECHAND NA ENDESH KATIKA WILAYA ZA KARATU NA MBULUUTAKAOGHARIMU KIASI CHA SHILINGI **83,225,177.00**
2. UCRT KWA UFADHILI WA UNOPS (UNITED NATIONS OFFICE FOR SMALL PROJECT SERVICES) LITATEKELEZA MRADI WA KUPANGA MATUMIZI YA ARDHI YA VIJIJI NA USIMAMIZI WA NYANDA ZA MALISHO KATIKA WILAYA YA MONDULI VIJIJI VYA LENGILORITI NA ENGORIKA UTAKAOGHARIMU SHILINGI **46,000,000**
3. UCRT KWA UFADHILI WA IRISH AID PROGRAME KUPITIA OXFAM TANZANIA ITATEKELEZA MRADI WA USAWA WA KIJINSIA, KUWAJENGEA WANAWAKE NA VIJANA UWEZO WA KIUCHUMI KATIKA WILAYA YA HANANG` VIJIJI VYA DANGAIDA, GARAWJA, WANDELA NA SAMSUMNGEJA UTAKAOGHARIMU SHILINGI **130,600,000.00**
4. UCRT KWA UFADHILI TOKA OXFAM TANZANIA ITATEKELEZA MRADI WA KUWAJENGEA UWEZO WANAWAKE NA VIJANA KIUCHUMI KATIKA WILAYA YA HANANG` KATIKA VIJIJI VYA GIDAMAMBURA, MULBADAW, GIDAGAMORI NA GASABOI UTAKAOGHARIMU SHILINGI **95,786,760.00**
5. UCRT KUPITIA UFADHILI TOKA THE NATURE CONSERVANCE ITATEKELEZA MRADI WA KUREJEA MIPANGO YA MATUMIZI YA ARDHI NAUSIMAMIZI WA NYANDA ZA MALISHO WILAYA YA LONGIDO KATIKA VIJIJI VYA MAGADINI, MEIRUGOI, ALAILILAI, MUNDARARA, RANCH, KISERIAN NA ENGIKARET UTAKAOGHARIMU SHILINGI **224,297,000.00**

MIRADI HII YOTE ITATEKELEZWA KWA KUSHIRIKIANA NA HALMASHAURI HUSIKA PAMOJA NA VIJIJI.

**KWA MAWASILIANO ZAIDI director@ujamaa-crt.org na manager@ujamaa-crt.org**

# Zitto amteua Membe Mshauri Mkuu ACT

**Na Waandishi Wetu**

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amemteua Waziri wa zamani wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, Bernard Membe, kuwa Mshauri Mkuu wa chama hicho, ikiwa ni wiki tatu tangu ajiunge nao rasmi Julai 16 mwaka huu.

Katika taarifa iliyotolewa jana na Naibu Katibu wa Uenezi, Habari na Mawasiliano kwa Umma ya chama hicho, Janeth Rithe, ilibainishwa kuwa, kwa mamlaka aliyopewa na katiba ya chama hicho kifungu cha 83(1)(d) ambacho kinampa mamlaka ya kuteua washauri wa chama, Zitto amefanya uteuzi huo, huku akimteua pia Emmanuel Mvula kuwa mjumbe wa Kamati Kuu ya chama. ACT-Wazalendo kwa sasa inaendelea na mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu na leo mkutano mkuu wa chama hicho unatarajiwa kujadili na kutangaza ilani ya chama hicho sambamba na kutangaza wagombea wa urais kwa pande zote mbili za muungano.

Hata hivyo, tayari kuna taarifa zinadai kuwa kuna mazungumzo yanaendelea baina ya chama hicho na vyama vingine vya upinzani kushirikiana katika uchaguzi huo.

Akizungumza katika kikao cha baraza kuu jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, alisema kuwa chama hicho kipo katika mazungumzo na ACT-Wazalendo, ili kuachiana maeneo ya kugombea ikiwamo nafasi ya urais kwa upande wa Zanzibar.

Membe tayari ameshachukua fomu ya kuomba ridhaa ya ACT-Wazalendo kuwania urais wa Tanzania katika uchaguzi huo uliopangwa kufanyika Oktoba 28, mwaka huu.

Vilevile, Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Sharif Hamad ameshachukua fomu na kurejesha kuwania urais wa Zanzibar kwa tiketi ya chama hicho.

***Imeandikwa na Enock Charles, Mary Mshami, Fatma Mtutuma na Magdalena Haule**



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda (kulia), akikabidhi vitendea kazi kwa Mkuu mpya wa Mkoa huo, Aboubakar Kunenge, katika hafla iliyofanyika jijini jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# NEC yaonya wasimamizi kuzima simu

**Na Waandishi Wetu**

WASIMAMIZI wa uchaguzi wa mikoa na wasimamizi wa uchaguzi mkuu ngazi ya wilaya na majimbo, wameagizwa kuhakikisha simu zao zinakuwa wazi katika kipindi chote hadi uchaguzi utakapomalizika na matokeo kutangazwa rasmi na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kadhalika, NEC imewasisitiza wasimamizi wa uchaguzi mkuu ngazi ya majimbo kutoka Shinyanga na Simiyu, wakasimamie vizuri uchaguzi huo ili ufanyike huru na haki, bila ya kusababisha dosari zozote zile ambazo zitaleta vurugu na kuchafua amani ya nchi.

Marufuku ya wasimamizi kutozima simu ilitolewa jana mjini Tabora na Ofisa wa NEC, Edward Makono, wakati wa mafunzo kwa wasimamizi wa uchaguzi 110 kutoka mikoa na Kigoma na Tabora.

Alisema lengo la kuwataka simu zao kuwa wazi ni kuhakikisha kuwa wanakuwa tayari kila wakati kupata maelekezo yanayohusu masuala ya uchaguzi na upokeaji wa vifaa vya uchaguzi vitakapoanza kugawiwa katika maeneo mbalimbali wanayosimamia.

"Mkiwa wasimamizi wa uchaguzi wanatakiwa kuwa tayari wakati wote hata ikibidi kupunguza baadhi ya shughuli binafsi ambazo zinaweza kuathiri uchaguzi...mnapolala lala ukiwa tayari na wala usizime simu yako wakati wote," alisisitiza.

Alisema kitendo cha kuzima simu kinaweza kusababisha msambazaji wa vifaa vya uchaguzi kuchelewa kufika katika vituo vinavyofuata, hivyo kuchelewesha uchaguzi.

Makono alisema msimamizi yeyote ambaye atasababisha vifaa vichelewe kupokelewa kutokana na simu yake kutopatikana, atachukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa umma na za NEC.

WAONYWA KUVURUGA AMANI

Katika hatua nyingine, NEC imewasisitiza wasimamizi wa uchaguzi mkuu ngazi ya majimbo kutoka Shinyanga na Simiyu, wasimamie vizuri ili ufanyike katika mazingira huru na haki, bila ya kusababisha dosari zozote zile ambazo zitaleta vurugu na kuchafua amani ya nchi.

Hayo yalibainishwa jana mjini Shinyanga na Kamishna wa NEC, Omari Ramadhan Mapuri, wakati akifunga mafunzo kwa wasimamizi wa uchaguzi mkuu wa mikoa ya Shinyanga na Simiyu.

Alisema hatima ya amani ya nchi kwenye uchaguzi mkuu ipo mikononi mwa wasimamizi, ambao wanapaswa kuzingatia sheria za uchaguzi pamoja na maelekezo ya tume ambayo wamepewa kwenye mafunzo, ili kufanikisha uchaguzi huo ufanyike kwa haki.

"Naombeni sana wasimamizi wa uchaguzi mkuu mzingatie mafunzo ambayo imepewa na tume, pamoja na kufuata sheria za uchaguzi, na kutofanya kazi kimazoea ili uchaguzi ufanyike kwa uhuru na haki,' alisema Mapuri.

"Kwenye changamoto kubwa ambazo hamna uwezo wa kuzitatua wasilianeni na tume zitatuliwe, ili kuepuka kujiingiza kwenye migogoro."

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Habari na Elimu ya Mpigakura wa NEC, Givness Aswile, aliwataka wasimamizi hao mafunzo ambayo wamepewa wayatoe pia kwa ufasaha kwa wasimamizi ngazi ya kata, ili uchaguzi ufanikiwe ngazi zote na kumalizika salama.

***Imeandikwa na Tiganya Vincent, TABORA na Marco Maduhu, SHINYANGA***

# Hatimaye Mwijako apata dhamana

**Na Hellen Mwango**

HATAMAYE msanii na Ofisa Masoko wa Clouds, Mwemba Burton, maarufu Mwijako (35), anayekabiliwa na mashtaka ya kusambaza picha za ngono kupitia mtandao wa WhatsApp, jana ametimiza masharti ya dhamana na ameachiwa na mahakama.

Dhamana hiyo imetolewa baada ya wadhamini Soud Kafio na Charles Mwendo, kufika jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate.

Hakimu alisema mshtakiwa ametimiza masharti ya dhamana na kwamba jukumu la wadhamini ni kuhakikisha anafika mahakamani kila kesi inapopangwa.

Alisema mshtakiwa yuko nje kwa dhamana mpaka Agosti 12, mwaka huu, kesi yake itakapotajwa.

Julai 29, mwaka huu upande wa Jamhuri ukiongozwa na mawakili wa Serikali Waandamizi, Wankyo Simon na Mwanaamina Kombakono, ulimsomea mshtakiwa mashtaka yake.

Kombakono alidai kuwa kati ya Septamba 17 na Oktoba 10, 2019, mshtakiwa alisambaza picha za ngono kupitia mtandao wa WhatsApp.

Mshtakiwa alikana shtaka hilo.

Wankyo alidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo uko mwishoni kukamilika na sehemu kubwa umeshakamilika.

Alidai kuwa Jamhuri haina pingamizi la dhamana, lakini waliomba mahakama itoe masharti yatakayompa mshtakiwa kuzingatia kufika kwenye kesi yake.

Wiki iliyopita Hakimu Kabate, alisema mahakama yake inampa mshtakiwa dhamana yenye masharti ya heshima na si ya kisaniisanii na kumtaka kuwa na wadhamini wawili kutoka Bongo Muvi au Bongo Fleva wenye barua kutoka Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA).

**Julai 29, mwaka huu upande wa Jamhuri ukiongozwa na mawakili wa Serikali Waandamizi, Wankyo Simon na Mwanaamina Kombakono, ulimsomea mshtakiwa mashtaka yake.**

## HABARI KITAIFA

# Mtaka ajivunia kuboreshwa maonyesho ya Nanenane

**Na Happy Severine, SIMIYU**

KUFANYIKA kwa maonyesho ya Nanenane kitaifa mkoani Simiyu kwa miaka mitatu mfululizo, kumeelezwa kumesaidia sana kuleta fikra mpya ya ushiriki na maandalizi ya maadhimisho ya Siku ya Wakulima nchini ambayo ni moja ya sherehe kubwa Tanzania.

Hayo yalibainishwa na Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, ambaye alibainisha kuwa kwao Nanenane si maonyesho tu ya kilimo bali ni fursa kubwa ya kilimo biashara yenye tija lukuki na inayolenga kuwajengea uwezo washiriki hasa wakulima, wafugaji na wavuvi

Mtaka aliongeza kuwa mtazamo huo mpya wa maonyesho ya kilimo na sherehe za wakulima nchini ni moja ya mafanikio ya kuandaa Nanenane kitaifa mkoani Simiyu tangu mwaka 2018.

Mtaka aliyabainisha alipotembea banda la Benki ya NMB ambayo alisema ni mdau mkubwa wa mafanikio yaliyopatikana na pia imechangia kwa kiasi kikubwa kubadilisha namna ya taasisi mbalimbali zinavyoshiriki kwenye maonyesho hayo na hasa ya mwaka huu.

"Kwa hiyo sisi kama mkoa hatusemi ni maonyesho ya kilimo tu ila tunasema ni maonyesho ya kilimo biashara kwa maana kwamba lengo lake ni kuwa na maonyesho ambayo wakulima na washiriki wengine wanakuja na mtazamo wa kuongeza thamani kwenye shughuli zao," aliongeza.

Alisema hiyo ilitokana na walichokiona na kujifunza walipokwenda Ufaransa, Rwanda na Afrika Kusini kama sehemu ya mkakati wa kujiandaa kuibadilisha Nanenane iwe ya manufaa zaidi kwa wakulima na kilimo pamoja na tija katika maendeleo ya taifa.

"NMB walituelewa na wametusaidia sana kufanikisha kuibadilisha Nanenane ambayo kufanyika kwake Simiyu tangu mwaka 2018 kumeleta mabadiliko makubwa sana na hii inaonyeshwa pia na hamasa kubwa waliyonayo wananchi ambao sasa hivi wanafika kwa wingi kwenye viwanja hivi vya maonyesho ukilinganisha na siku za nyuma," alisema Mtaka.

Alisema walipoanza kutekeleza mpango wa kuwajengea washiriki uwezo na kuwasaidia kuongeza thamani waonyeshaji, NMB ilikuwa peke yake kuusaidia mkoa kufanikisha malengo hayo, lakini sasa hivi kila benki na wadau wengine wanafanya hivyo.

"Hii ni pamoja na kutoa mafunzo maalumu na elimu kwa makundi mbalimbali wakati wa maonyesho na kuwawezesha wale ambao wamewaunga mkono na kuwasaidia kukua kushiriki ili wawe mashuhuda wa mafanikio yanayopatikana."

Akizungumzia mafunzo yanayotolewa na Benki ya NMB kwenye banda lao, kiongozi wa ushiriki wa benki hiyo, ambaye ni Meneja wa NMB Kanda ya Magharibi, Sospeter Magese, alisema mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa tangu mwaka 2018 kuwaelimisha wakulima waweze kukua kupitia benki hiyo kubwa nchini. Alisema walianza kwa kutoa mafunzo kwa vyama 20 vya ushirika wa wakulima na idadi hiyo iliongezeka hadi vyama 30 mwaka jana, huku mwaka huu wakitarajia kutoa elimu ya fedha na mafunzo ya biashara kwa vyama 40.

Alisema msingi wa mafunzo wanayopewa wakulima ni elimu ya biashara kilimo ili waweze kukifanya kilimo chao kiwe cha kibiashara zaidi na waweze kuwekeza kukiboresha na kukifanya kiwe cha kisasa kwa manufaa zaidi.

# SUMAJKT yanunua magari, pikipiki kujiimarisha

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMAJKT), kupitia kampuni zake mbili SUMAJKT Guard na inayojishughulisha na usafi, zimezindua magari na pikipiki ya kujiimarisha kiutendaji.

Vifaa hivyo, vinatokana na Sh. milioni 353.6 zilizotengwa na shirika hilo kuimarisha huduma ya vifaa kwa kampuni hizo.

Uzinduzi wa vifaa hivyo ulifanywa jana na Mwakilishi wa Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Brigedia Jenerali, Charles Mbunge ambaye ni Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa SUMAJKT anayeshughulikia Utawala, Kanali Absolomoni Shausi.

Brigedia Jenerali Mbunge alisema kupitia shirika hilo ametenga Sh. milioni 353.6 kwa lengo la kuimarisha kampuni hizo kivifaa.

"Vifaa hivi vinanunuliwa ili kuhakikisha miradi yote iliyopo chini ya shirika inapata vitendea kazi, kuongezeka kwa vitendea kazi kunaashiria ongezeko la wateja, malindo na ajira zimeongezeka," alisema.

> **"Vifaa hivi vinanunuliwa ili kuhakikisha miradi yote iliyopo chini ya shirika inapata vitendea kazi, kuongezeka kwa vitendea kazi kunaashiria ongezeko la wateja, malindo na ajira...**

Aliwataka watendaji wanaosimamia miradi hiyo kuhakikisha vifaa hivyo vinatunzwa na madereva wahakikishe magari wanayokabidhiwa yanaleta faida na kukaa muda mrefu.

"Tunazihakikisha taasisi mbalimbali, sekta binafsi na watu binafsi ambao wanatumia huduma zetu kuwa tutaendelea kuzitoa kwa ubora zaidi na kwa wakati," alisema.

Naye Mkurugenzi Mwendeshaji wa kampuni hiyo, Luteni Kanali, Joseph Masanja alisema mpaka sasa wana zaidi ya magari 40 na pikipiki zaidi ya 80 na hivi karibuni walinunua magari 11 kwa ajili ya usafi na ulinzi.

Alisema changamoto inayowakabili ni wateja kuchelewa kulipa ingawa jambo hilo serikali ilishalitolea maelekezo.

Alisema kampuni ya ulinzi wakati inaanza kazi mwaka 2010 baada ya usajili wake uliofanyika Oktoba 20, mwaka 2008, ilikuwa na walinzi saba, lakini kwa sasa wamefikia 11,214 na miongoni mwao wanawake ni 2,899.

Naye Meneja wa Kampuni ya usafi na unyunyiziaji dawa, Kapteni Rosemary Katani, alisema mradi umefanikiwa kununua magari mawili aina ya Canter ya tani 3.5 kwa Sh. milioni 55 na Tipper la tani 10 kwa Sh. milioni 103 kwa ajili ya kuzoa taka.

Alisema mradi umeajiri vibarua 448 wa kazi za usafi, umetengeneza sabuni kwa matumizi yao na wateja wa nje na kutengeneza vyungu vya kupandia maua.

Pia alisema kampuni ya usafi na unyunyiziaji dawa imeongeza washiriki kutoka 10 hadi 16 katika taasisi za serikali.


Tanzania Forest Conservation Group

**EMPLOYMENT OPPORTUNITY**

The Tanzania Forest Conservation Group (TFCG) is a national NGO whose mission is to reduce poverty in rural communities and to conserve the biodiversity of globally important forests in Tanzania for the benefit of the present and future generations. TFCG, in partnership with the Community Forestry Network of Tanzania (MJUMITA) is implementing the Eco-schools in Africa Programme – Tanzania. The position is financed by DANIDA through the Danish Outdoor Council. The overall programme objective of the Eco- School is: to promote active citizenship and improved livelihoods through Education for Sustainable Development.

As part of this project, TFCG is seeking applications from qualified Tanzanian women and men for the following position:

**Assistant Environmental Education Officer, Dar es Salaam**

**Responsibilities**

- The Assistant Environmental Education Officer will implement specific programme activities in accordance with the work plan and budget submitted by TFCG to DOC with a specific focus on Component 1 of the project. This is the Capacity building Component. The Assistant Environmental Education Officer will assist in building the capacity of primary and secondary school teachers and local government staff to deliver quality education for sustainable development.
- The Assistant Environmental Education Officer shall provide detailed and accurate reports on any programme expenditure for which s/he is responsible in accordance with TFCG financial guidelines.
- To assist in monitoring and documenting the programme's activities using the indicators outlined in the logical frame work.

**Qualifications and experience**

- BSc. in a related discipline such as Forestry, Education, Biological sciences, Environmental sciences or B.Ed.
- Formal training on a rights-based approach to education is preferred.
- At least 3 years relevant practical experience in the field of education for sustainable development including work with schools, rural communities and local authorities.

**How you can apply**

The Job Description and other details are available at: **http://www.tfcg.org/careers.html**

Qualified candidates should send applications including CV, covering letter, contact details (including an e-mail address and phone number) and contacts of three professional referees to: **personnel@tfcg.or.tz**

**The deadline for applications is 04:00pm on 15th August, 2020.**

215842302

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi wasimuachie Rais kutatua kila kero

**MAMBO** ambayo wengi bila shaka watakuwa waliyaona wiki iliyopita wakati Rais John Magufuli akirejea jijini Dar es Salaam akitokea wilayani Masasi mkoani Mtwara kwenye maziko ya Rais wa Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, yamedhihirisha kuwa uwajibikaji bado ni tatizo kwa viongozi wengi wa umma.

Rais Magufuli aliamua kutumia usafiri wa barabara kupitia wilaya kadhaa za mikoa ya Lindi na Pwani kwa lengo la kuzungumza na wananchi pamoja na kusikiliza kero zao.

Kuanzia Somanga mkoani Lindi hadi Mkuranga, mkoani Pwani, wananchi walimweleza Rais kero ambazo katika hali ya kawaida zilitakiwa utatuliwa na viongozi wa maeneo hayo kama wakuu wa wilaya, wakurugenzi, wabunge na makatibu tawala wa wilaya husika.

Kero hizo zilijikita katika migogoro ya wakulima na wafugaji, wafanyabiashara kukosa vyoo kwenye masoko, uchakavu wa shule na uhaba wa madawati, kukosekana kwa mabari ya kubebwa wagonjwa, kutojengwa kwa kituo cha afya licha ya serikali kupeleka fedha na viongozi kukosa magari.

Kila Rais magufuli alipokuwa akipokea kero za wananchi na kuwaita viongozi kuzijibu, ilionekana dhahiri kuwa hawakuwa na majibu sahihi, hali iliyokuwa ikimfanya Rais kushangaa.

Jambo la kushangaza ni viongozi husuan wa kuteuliwa nawafanya nini katika maeneo yao ya utawala kama hawafahamu kero za wananchi kisha kuwajibika kwa kuzipatia ufumbuzi.

Kama viongozi hao wanakaa maofisini badala ya kuwafuata wananchi na kuwaulizia kero zao, ina maana hakuna wanachoisaidia serikali, ambayo ndiyo inayowalipa mishahara kila mwezi.

Tatizo tunaloliona ni kuwa viongozi wetu wengi katika ngazi mbalimbali wanashindwa kubadilika kiutendaji, badala yake bado wanaendelea na fikra zile zile za zamani za kufanya kazi kwa mazoea bila kujua kuwa enzi hizo zimepitwa na wakati.

Kinachotakiwa kwa sasa ni viongozi kuwa wabunifu, wachapa kazi kwa tija na ufanisi kwa kuwa mwisho wa siku kinachowapima ni utendaji wao.

Bila hivyo, tutaendelea kuwashuhudia watu wakikaa tu vijiweni wakisubiri kuteuliwa kuwa wakurugenzi, wakuu wa wilaya, makatibu tawala, wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa bila kujua kuwa kukimbilia huko katika awamu hii ya uongozi hakuna kudekezana wala kubembelezana isipokuwa adhabu ya kushindwa kuleta matokeo ni kutumbuliwa.

Ingawa baadhi ya watu wanalalamikia utumbuaji wa majipu, lakini kimsingi hiyo ndiyo dawa kwa viongozi wanaoshindwa kutekeleza wajibu wao na kuwasubiri viongozi wa kitaifa kutatua kero za wananchi wakati ni majukumu yao.

Hatutarajii tena kuwaona wala kuwasikia viongozi wanaoshindwa kutatua migogoro ya wafugaji na wakulima katika maeneo yao wakati hilo ni jukumu lao la msingi, tena ndio wanaoziongoza kamati za ulinzi na usalama kwenye maeneo yao ya kiutawala.

Kwa upande mwingine, viongozi katika ngazi za wilaya na halmashauri wanapaswa kujiongeza kwa kuwa wabunifu kwa kuongexa vyanzo zaidi vya mapato. Kwa mfano, ni jambo lisiloeleweka kuwasikia wakuu wa wilaya na wakurugenzi kuwa wafanyabiashara kwenye masoko hawana huduma za vyoo.


Halmashauri zinaweza kujenga vyoo kwa vyanzo vyaka vya mapato kisha kuweka tozo kwa watumiaji, hivyo fedha hizo kurudia kama mapato yake. Wakati mwingine halmashauri inaweza kuwapa zabuni wawekezaji kutoa huduma hiyo kisha nayo kulipwa tozo.

Tunaona kuwa utaratibu wa Rais Magufuli kupita kwa wananchi anapopata fursa na kuwasikiliza, itamsaidia zaidi kuwabaini wateule wake kama wanatekeleza wajibu wao ipasavyo na kuwaondolea kero wanyonge, ili wasiofanya hivyo watumbuliwe.

Tunaamini kuwa hatua hiyo itawafanya viongozi wenye dhamana kuchacharika kutekeleza majukumu yao ya msingi ya kuwaondolea kero wananchi wanyonge.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Ulinzi mabinti uanze kudhibiti utumikishwaji wa nyumbani

Fatma Mtutuma na Faudhia Sultan (UDOM)

WATOTO wengi wa kike sehemu nyingi duniani wanakabiliwa na vikwazo kama kutothaminiwa katika jamii pale wanapoanzisha safari yao ya kuelekea utu uzima.

Kutokana na vikwanzo hivyo wanavyokutana navyo ambavyo ni pamoja na mimba na ndoa za ututoni, unyanyasaji,ubakaji pamoja na kutokuwa na usalama wa kutosha katika jamii., wengi hawajui hatima yao.

Mabinti wanakabiliwa na changamoto nyingi. Kiini chake ni kukosekana kwa usawa wa kijinsia pamoja na usalama katika jamii nyingi hasa za Kiafrika yakiwamo makabila mengi ya Tanzania .

Hali hiyo huwakuza na kuwainua watoto wa kiume na kuwadhalilisha wa kike kuanzia ngazi ya familia hadi taifa.

Ipo dhana potofu katika jamii ya wengi kuamini kuwa mtoto wa kike hawezi kufanya jambo la muhimu ikilinganishwa na watoto wa kiume. Dhana hiyo hutokana na mfumo dume uliotawala katika jamii nyingi ambazo zinaamini kuwa watoto wa kiume ni muhimu zaidi na hivyo hupewa kipaumbele na fursa katika nyanja zote ikiwamo kipaumbele katika kupata elimu.

Ubaguzi huo huchangia mabinti kulazimishwa kuacha masomo na kukatisha ndoto zao.

Hivyo umewadia wakati wa dunia kuchukua hatua na kuwapa fursa ya maisha bora wasichana hawa pamoja na kuwawezesha kutimiza ndoto zao katika jamii wanazoishi.

Hata hivyo changamoto zinazowakabili wasichana zinatatulika kwa kuimarisha uwezo wao wa kujiamini.

Baadhi ya njia ambazo zinaweza kutatua changamoto hizo ni pamoja na

elimu kupewa kipaumbele hasa kwa mtoto wa kike.

Serikali, wazazi , walezi na walimu wanatakiwa kufanya bidii ili kuleta usawa baina ya wavulana na wasichana kwenye elimu.

Aidha, kuwahamaisha kupenda elimu na kuwapa moyo katika masomo yao ni mojawapo ya mbinu za kumuimarisha mtoto wa kike, kwani atajiona yuko sawa na wenzake wa kiume.

Halikadhalika elimu ya utambuzi ni muhimu kwa wasichana, wanatakiwa kukumbushwa kuwa ni sehemu ya jamii na hivyo kazi yao sio kuzaa pekee.

Hivyo hamasa hiyo inatakiwa kufikishwa kwa nguvu zote kwa jamii zote zisizothamini kuwasomesha, kuwaoza .

Mtoto wa kike anatakiwa aelimishwe kuwa anawajibika kujenga jamii yake kwa namna nyingi si kuzaa pekee. Aidha, atambue mchango wake kwa jamii kiuchumi na kisiasa.

Kampeni zinaweza kusaidia wanajamii kuondokana na dhana potofu ya kuwa mtoto wa kike hana thamani sawa na mtoto wa kiume.

Asasi mbalimbali za kiserikali na kiraia zinaweza kutoa elimu kwa jamii kuhusu thamani ya watoto wote, wa kike na wa kiume.

Vilevile, wazifahamishe jamii namna ya kuripoti matukio yanayohusu unyanyasaji wa mtoto wa kike.

Aidha, ili kudhibiti utumikishwaji wasichana, ajira ya wasichana wa ndani iangaliwe upya na

Ni muhimu pia taifa likaweka sheria inayoelekeza au kutoa mwongozo wa ajira za wasichana wa ndani.

Kwamba sheria itamke wazi kuwa msichana aliye chini ya miaka 18 asiajiriwe kufanya kazi za ndani. Hii itachangia jamii nzima kumthamini mtoto wa kike na kumuongezea nafasi mtoto wa kike kufikia ndoto zake.

Pengine wakati umefika kwa kila mmoja kutumia nafasi aliyonayo iwe nyumbani, shuleni, kazini, ama katika jamii; kuondoa changamoto zinazomkabili msichana kutokana na ubaguzi.

Walimu na walezi maana wao hutumia muda mwingi na watoto na wanaweza kuwajengea dhana chanya ya usawa wa kijinsia wakiwa na umri mdogo.

## HABARI PICHANI

# MATUKIO YA BARAZA KUU LA CHADEMA KATIKA PICHA



Viongozi wakuu wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakiongozwa na Mwenyekiti wa Taifa, Freeman Mbowe (kushoto) na Makamu Mwenyekiti Bara, Tundu Lissu (wa pili kushoto), wakiingia katika Ukumbi wa Mliman City, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya mkutano wa Baraza Kuu la chama hicho. **PICHA ZOTE: ANTHONY SIAME**




Viongozi wakuu wa chama hicho, wakiimba wimbo wa Taifa wakati wa mkutano huo.



Wajumbe wa Mkutano wa Baraza Kuu wakiimba wimbo wa Taifa.



Viongozi wakuu wa chama hicho, wakiomba dua wakati wa Mkutano wa Baraza Kuu la CHADEMA.



Sehemu ya wajumbe wa Mkutano huo, wakiwa ukumbini.



Wanaowania kuteuliwa kugombea urais kupitia chama hicho, Tundu Lissu (kushoto), Lazaro Nyalandu (katikati) na Maryrose Majinge wakiwa kwenye mkutano wa Baraza Kuu.

# Mahari kubwa chanzo cha ukahaba wasichana

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

UTOZAJI wa mahari kubwa kwa baadhi ya wazazi husus an jamii za kifugaji, umetajwa kusababisha baadhi ya watoto wa kike kushindwa kuolewa na wanaume na kujiingiza katika biashara ya ngono na uzazi holela, imeelezwa.

Hali hiyo imeelezwa kuwa imekuwa ikisababisha uwapo wa watoto wengi wasio na baba, wanaolelewa na bibi zao kutokana na kuzaliwa nje ya ndoa baada ya wazazi kuwa na tamaa ya kuwafanya mabinti zao kama kitega uchumi kwa kuwatoza mahari kubwa vijana wanapojitokeza kuwaposa na kushindwa kumudu gharama hiyo.

Hayo yalibainishwa jana na baadhi ya washiriki wa warsha ya siku moja ya kujadili na kuunda sheria ndogo ndogo zinazomlinda mwanamke na mtoto dhidi ya mila na desturi potofu zinazosababisha ukatili wa kijinsia. Semina hiyo iliandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la HUHESO Foundation kwa ufadhili wa The Foundation for Civil Society (FCS).

Mary Chima, Ofisa Maendeleo ya Jamii wa Halmashauri ya Mji wa Kahama, alisema utozaji mkubwa wa fedha za mahari kwa baadhi ya wazazi na walezi, umekuwa ukichangia kwa asilimia kubwa vijana kushindwa kumudu gharama na kusababisha mabinti kujiingiza kwenye biashara haramu ya ngono.

"Hatuwazuii wazazi kutoza mahari kubwa kwa mabinti zao, lakini tuangalie kama mahali tuliyoitaja anayekwenda kuoa anaweza kuimudu. Vijana wengi wanashindwa kuoa baada ya kutozwa kiasi kikubwa na kusababisha binti kujiingiza kwenye biashara haramu na kuzaa watoto na kuwatelekeza," alisema Chima.

Naye Joel Mracha, Ofisa Sheria alisema mwanamke anapofiwa na mwenza wake ana haki ya kuishi popote, lakini baadhi ya makabila yamekuwa yakimtafutia mrithi ambaye ni mdogo au mkubwa wa marehemu na kuanza kunyanyasika na wengine kuchukua jukumu la kukimbia familia.

Mkufunzi katika warsha hiyo ambaye Ofisa Ustawi wa Jamii, Halmashauri ya Mji wa Kahama, Abdulrahman Nuru, alisema jamii nzima inapaswa kuelewa na kuzipinga mila na desturi kandamizi zilizoko katika jamii ili kuwalinda wanawake na watoto dhidi ya ukatili.

Pia alisema ni muhimu serikali na mashirika binafsi kuendelea kutoa elimu kwa jamii kufuata sera na sheria zinazowalinda wanawake na watoto dhidi ya ukatili wa kijinsia. Pia aliwataka wazazi kuacha kutoza mahari kubwa ambayo itamfanya mtoto wa kike kuolewa na anayemtaka.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, anayeshughulikia Uwekezaji, Angellah Kairuki (wa pili kushoto), akimsikiliza Ofisa Uhusiano Mwandamizi wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Sebera Fulgence, wakati alipotembelea banda la Mfuko huo, kwenye maonyesho ya wakulima Nanenane katika viwanja vya Nyakabindi wilayani Bariadi, mkoani Simiyu, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Apigia debe unyonyeshaji mtoto maziwa ya mama

**Na Steven William, MUHEZA**

MKURUGENZI Mtendaji Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania (TFNC), Dk. Germana Leyna, amewasisitiza kinamama kujenga tabia ya kunyonyesha watoto wachanga.

Amesema maziwa hayo ni muhimu kwa kuwa yana virutubisho vyote vinavyohitajika kwa mtoto ili kumjenga kiakili katika ukuaji wake na kutengeneza uhusiano wa karibu kwa mama na mtoto.

Dk. Leyna alisema hayo juzi mbele ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, wakati wa uzinduzi wa Maadhimisho ya Wiki ya Unyonyeshaji Duniani yaliofanyika kitaifa katika Uwanja wa Jitegemee, wilayani hapa.

Alisema kushindwa kumnyonyesha mtoto kuna madhara kiafya na kimwili ikiwamo mtoto kupata udumavu wa akili, uwezo mdogo wa kufikiri na akiwa shuleni atakuwa hana akili ya kufanya vizuri darasani.

Leyna alisema madhara ya kumpa chakula mtoto akiwa mdogo yanaweza kusababisha kupata utapiamlo na kwamba akinyonyeshwa vizuri kuna faida ikiwamo kujenga afya bora na kuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri.

Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Mhandisi Mwanasha Tumbo, alisema maziwa ya mama ni muhimu kumnyonyesha mtoto moja kwa moja na husaidia kuzuia mimba nyingine kwa mama.

Alisema katika Wilaya ya Muheza kuna watoto 822 wenye ulemavu na kati ya hao 244 wana ulemavu mkali na wanashindwa hata kwenda shuleni kusoma, hivyo wameamua kujenga mabweni matatu kwa ajili ya watoto hao na sasa yamefikia hatua za mwisho. Tumbo alisema kuwa watoto wilayani Muheza waliopata ulemavu na udumavu, wazazi wao wanawanyonyesha kwa asilimia 70 na kwamba wataalamu wanaendelea kutoa elimu kwa wazazi wao, huku akiwataka kinababa wajenge tabia ya kwenda kliniki na wake zao.

## Taasisi yawezesha 70 kusoma vyuo nje

**Na Mwandishi Wetu**

TAASISI ya Study Abroad Universities, imewaunganisha zaidi ya wanafunzi 70 kusoma vyuo vikuu na fani mbalimbali nje ya nchi.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Meneja wa taasisi hiyo Mkoa wa Dar es Salaam, Mohamed Lucas, wakati akizungumzia mafanikio waliyopata tangu kuanzishwa kwake.

Alisema waliwaunganisha wanafunzi hao na vyuo vikuu kwenye nchi za China, India, Uingereza, Malaysia, Cyprus, Ukraine na Canada na kwa upande wa Afrika Mashariki wamewapeleka kusoma Uganda.

Mbali na kuwanganisha wanafunzi hao na vyuo hivyo, alisema wamekuwa wakiwafuatilia kujua maendeleo yao kitaaluma na kama wanakabiliwa na changamoto ili wazitatue.

Alisema hadi sasa wanafunzi wao hawajapata changamoto yoyote kwenye vyuo walivyowapeleka kwa kuwa kwa kawaida wanashirikisha Tume ya Vyuo Vikuu (TCU) ili kujua kama vyuo hivyo vinatambulia.

Lucas alisema wamekuwa pia wakiwashauri wanafunzi fani za kusoma kulingana na masomo waliyochukua na kwamba mwaka huu wa masomo wanatarajia kuwapeleka kwenye vyuo hivyo nje ya nchi zaidi ya wanafunzi 100.

Kuhusu kuwapatia mikopo wanafunzi wenye changamoto hiyo, Lucas alisema wako kwenye mazungumzo na baadhi ya taasisi za fedha ili kuangalia uwezekano wa kufanikisha jambo hilo.

"Tuko katika hatua nzuri ya mazungumzo na tungependa kuona tunawasaidia wanafunzi wenye changamoto ya ada wapate mkopo hivyo tutakapofikia makubaliano tunawaarifu," alisema

Lucas aliongeza kuwa wana matawi Arusha na Zanzibar

Alisema taasisi hiyo imekuwa ikifanya tafiti kujua vyuo sahihi vya kuwapeleka wanafunzi wanaotaka kusomea fani mbalimbali wanapomaliza kidato cha sita.

"Kwa mfano wanafunzi wengi kama siyo wote wanaopenda kusomea udaktari na fani ya utabibu huwa tunawaunganisha na vyuo vya China, India na Ukrane maana kule ndiko tumeona ni sehemu sahihi kwa fani yao," alisema Lucas.

HABARI KITAIFA

# Akaunti ya NBC yavutia wadau kilimo Nanenane

**Na Mwandishi Wetu**

WADAU mbalimbali wa kilimo wanaoshiriki na kutembelea Maonyesho ya Kilimo ya NaneNane yanayofanyika kitaifa kwenye Uwanja wa Nyakabindi, Bariadi mkoani Simiyu, wameonyesha kuvutiwa na huduma mpya ya NBC Shambani ambayo imebuniwa mahususi kwenda sambamba na mahitaji ya huduma za kifedha ya wadau hao.

Akifafanua kuhusu huduma hiyo mpya kwa wadau mbalimbali waliotembelea banda la benki hiyo kwenye maonyesho hayo, Mkuu wa kitengo cha wateja wadogo na wakati, kutoka benki hiyo, Raymond Urassa, alisema inalenga wadau wote wanaojihusisha na biashara ya kilimo wakiwamo wasambazaji wa pembejeo za kilimo, wakulima na wasafirishaji wa mazao ya kilimo.

"Lengo hasa la huduma hii ya NBC Shambani ni kuwasaidia wadau wa kilimo kutimiza malengo yao ya biashara ya kilimo ambapo inatoa fursa kwao kuwa na akaunti ya vikundi vya wakulima kama vile AMCOS na vikundi vingine pamoja na akaunti ya mkulima mmoja mmoja," alisema.

Mbali na kuwawezesha wakulima hao kutunza fedha zao kwa urahisi, Urassa alizitaja baadhi ya faida za huduma hiyo kwa mkulima mmoja mmoja kuwa ni pamoja na mkulima kupata faida kwa salio la akiba linalozidi Sh. 100,000 na kuendelea huku pia kukiwa hakuna makato ya kila mwezi.

"Akaunti ya NBC Shambani kwa vikundi vya wakulima inawawezesha kuweka fedha bila ada ya uendeshaji wa akaunti huku pia vikundi vikifaidika kwa faida nyingi ikiwamo kutokatwa gharama za uendeshaji wa akaunti kila mwezi, kupata taarifa za akaunti bure sambamba na kutokatwa makato ya kuhamisha fedha wakati wa kulipa wakulima wenye akaunti NBC," alifafanua.

Wakizungumzia huduma hiyo, baadhi ya wadau wa kilimo walisema imekuja wakati mwafaka kwa kuwa kwasasa taifa linapitia mageuzi ya kilimo ambayo ustawi wake kwa kiasi kikubwa unategemea uwapo wa huduma bora za kibenki zinaenda sambamba na mahitaji ya wadau hao.

# Mbaazi kuuzwa kwa stakabadhi ghalani

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

**Kupitia utaratibu huo, wakulima watatakiwa kuzingatia usafi, kutouza mbaazi zenye unyevu mwingi kwenye mazao yao, hali itakayowafanya waweze kuuza zikiwa katika daraja la kwanza.**

WADAU wa zao la mbaazi wilayani Tunduru mkoani Ruvuma wamekubaliana kuanza kuuza zao hilo kupitia utaratibu wa stakabadhi ghalani ikiwa ili kuunga mkono juhudi za serikali za kuongeza thamani ya mazao ya wakulima kuanzia msimu wa mwaka 2019/2020.

Makubaliano hayo yalifikiwa kufutia kikao cha wadau wa zao hilo kilichofanyika Tarafa ya Mlingoti wilayani hapa, na kwamba utaratibu huo utasaidia kukuza vipato vya wakulima wa zao hilo kama ilivyo kwenye mazao ya korosho na ufuta.

Aidha, kupitia tamko hilo, viongozi wa vyama vya msingi vya wakulima AMCOS wilayani humo wametakiwa kwenda kwa wakulima kutoa elimu na kuanza kukusanya mazao ya wakulima kupitia vyama vyao kuanzia wiki hii, na kwamba mnada wa kwanza wa kuuza mbaazi zao utapangwa kufanyika wakati wowote kuanzia wiki ijayo.

Awali, mwakilishi wa Ofisa Kilimo wa Wilaya ya Tunduru, Raymond Rafael, alisema kupitia utaratibu huo, wakulima watatakiwa kuzingatia usafi, kutouza mbaazi zenye unyevu mwingi kwenye mazao yao, hali itakayowafanya waweze kuuza zikiwa katika daraja la kwanza.

Ofisa Mazao wa Wilaya ya Tunduru, Gallus Makwisa, alisema maamuzi hayo yametokana na idara yake kubaini uwapo wa ubabaishaji wa soko la zao hilo, hali inayoonyesha kuwakatisha tamaa wakulima wengi kuendelea na kilimo cha zao hilo.

Meneja wa Chama Kikuu cha Ushirika wa Wakulima Wilaya ya Tunduru (TAMCU), Imani Kalembo, alisema baada ya wadau hao kupitisha kuanza kwa utaratibu wa kuuza mbaazi kupitia utaratibu wa mfumo wa stakabadhi ya mazao ghalani, TAMCU itafanya utaratibu wa kuagiza vifungashio vya kubebea mazao hayo kwa haraka ili kutoa nafasi kwa viongozi wa vyama vya msingi kuanza kukusanya mbaazi za wakulima kuanzia Agosti 6, mwaka huu.

Akifungua kikao hicho Mkuu wa Wilaya ya Tunduru, Julius Mtatiro, aliwataka wajumbe hao katika mjadala kujielekeza katika uainishaji wa changamoto ili viongozi watakaosimamia utaratibu huo kuwa na majibu wakati wa utekelezaji wake.

Alisema katika utekelezaji huo, serikali imejipanga kuhakikisha kuwa hakuna mkulima ambaye ataibiwa mazao yake na viongozi wa vyama hivyo pamoja na kuhakikisha wanunuzi wa mazao hayo wanalipa fedha ndani ya muda mfupi baada ya kununua mazao ya wakulima.



Kaimu Meneja wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Nyaswi Elias (kushoto), akimuhudumia mwanachama wa mfuko huo, aliyetembelea banda la mfuko huo, katika maonyesho ya Nanenane kwenye viwanja vya Nyakabidni nje kidogo ya mji wa Bariadi, mkoani Simiyu, jana. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Zaidi ya kaya 2000 maskini kuhakikiwa TASAF

**Na Elisante John,** SINGIDA

ZAIDI ya kaya 2,800 maskini katika Manispaa ya Singida zinazonufaika na ruzuku kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii nchini (TASAF), zitahakikiwa ili kuiwezesha serikali kupata taarifa sahihi zaidi zitakazotumika kwenye mipango ya maendeleo.

Mpango huo unaotekelezwa nchini na TASAF awamu ya tatu, katika hatua ya pili, unaelezwa utazingatia zaidi umuhimu wa takwimu sahihi zitakazopatikana kwenye kaya husika, ili kutimiza lengo la serikali, katika kunusuru familia za walengwa kuhusu ukubwa wa tatizo hilo.

Akizungumza wakati wa mafunzo ya siku mbili kwa watumishi wa manispaa hiyo watakaohudumia zoezi hilo, Mkuu wa kitengo cha mawasiliano kutoka TASAF, Zuhura Mdungi, alisema uhakiki huo utatambua orodha halisi ya walio na sifa ya kuingizwa katika mpango.

Alisema, iwapo mlengwa ataamua mwenyewe kujitoa kwa hiari kwenye mpango wakati wa zoezi hilo, maofisa wa uhakiki wanapaswa wakubaliane na uamuzi wake, ili kuondoa mgongano.

"Nisisitize tu kuwa, pia kaya ambazo hazijahakikiwa, zitakuwa nje kwa muda hadi pale mhusika atakapokamilisha taratibu za uhakiki...sisi kazi yetu ni kutekeleza tu, atakayekubali kuhakikiwa ni yule mwenye kitambulisho cha mpango wa TASAF," alifafanua Mdungi.

Katika hatua nyingine mwezeshaji wa mafunzo hayo kitaifa, Sekella Komba, alisema zamani mpango wa TASAF ulihusisha halmashauri za wilaya 131 nchini kote, lakini kwa mpango wa sasa zitaongezeka na kufikia 187, zikiwamo pia za Unguja na Pemba.

Aliwataka wasimamizi wa mpango huo, kuelimisha walengwa kwa kiwango cha juu, na kutoa nafasi kwa watakaoamua kujitoa kwa hiari wakubaliwe, na hata kaya ambazo zimepiga hatua ya kukabiliana na umaskini kwa kuwa na viongozi wa kijamii, nazo zikubaliwe kujitoa.

Wahakiki pia wametakiwa kutumia vyema dodoso la uhakiki, kwa kuwa baada ya kukamilisha kazi hiyo, ndilo litakalotumika pia kupitia mfumo kuamua mlengwa gani anastahili kuendelea kwenye mpango kwa kutegemea taarifa sahihi.

Manispaa ya Singida yenye vijiji na mitaa 27, ina kaya 2,801 zinazohudumiwa na TASAF, huku ikielezwa hadi kufikia Januari mwaka huu, kaya 36,136 za vijiji 278 vya Mkoa wa Singida, zimenufaika na ruzuku ya zaidi ya Sh. bilioni 42.2 kukabiliana na umaskini uliokithiri.

# Wasichana washinda tuzo ya wanasayansi chipukizi

**Na Elizabeth Zaya**

WANAFUNZI wawili wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Nganza ya Mkoa wa Mwanza wameibuka washindi wa jumla wa tuzo ya mwaka ya wanasayansi chipukizi Tanzania (YST), ambayo hufanyika kila mwaka.

Wanafunzi hao waliibuka kidedea baada ya ugunduzi wao wa kisayansi ambao ulisaidia katika uzalishaji wa samaki kwa haraka katika shule yao pamoja na mifugo mingine. Baada ya wanafunzi hao kuibuka kidedea, walizawadiwa tuzo na medali za kikombe pamoja na fedha taslimu Sh. milioni 1.35.

Wanafunzi hao ni Glory Kiroche na Martha Machumu, ambao pia mbali na kupatiwa medali, watadhaminiwa masomo yao ya chuo kikuu kutoka kwa Taasisi ya Karimjee Jivanjee Foundation.

Katika kukamilisha utafiti huo, wanafunzi walitumia muda wao katika kutafiti lishe bora na inayofaa kwa mifugo pamoja na mazao ya kilimo.

**Na tulivyojaribu njia hii ilionekana ni bora kuliko kutumia majani ya kawaida na baadaye tuligundua kwamba siyo kwa wanyama tu hata katika kuzalisha mazao ya kilimo.**

Glory alisema chakula hicho kilikuwa kinazalishwa kwa siku sita mpaka saba tu na kuanza kutumika kwa mifugo na walikuwa wakitumia maji na nafaka pekee kukitengeneza kwa kurutubishwa na mbolea ya wanyama.

"Kwa mfano ng`ombe wa maziwa, chakula hiki kinasaidia kuzalisha maziwa mengi zaidi, kama ulikuwa unazalisha lita tano, utazalisha mara mbili yake na pia na inasaidia kuongeza uzito kwa mifugo kuliko kutumia majani ya kawaida," alisema Grory.

Alisema walipata wazo la kubuni teknolojia hiyo baada ya kupata shida na kutumia gharama kubwa kuhudumia mifuko katika shule yao.

"Tulipata wazo kwa sababu shuleni tulikuwa tunatumia gharama kubwa kununua chakula cha mifugo, kwa hiyo ndipo tulipata akili ya kugundua teknolojia hiyo na ilitusaidia sana katika kulisha na kuzalisha samaki kwa wiki shuleni kwetu," alisema Groly.

"Na tulivyojaribu njia hii ilionekana ni bora kuliko kutumia majani ya kawaida na baadaye tuligundua kwamba siyo kwa wanyama tu hata katika kuzalisha mazao ya kilimo."

Mwenyekiti wa Bodi ya YST, Prof. Yunus Mgaya, alisema maonyesho ya 2020 YST yalijumuisha miradi zaidi ya 6,000 kutoka maeneo mbalimbali ikiwamo upande wa sayansi, sayansi ya hesabu, sayansi ya kibaolojia na ikolojia, sayansi ya kijamii na teknolojia.

Mwanzilishi wa Tuzo hizo za YST, Dk. Gozbert Kamugisha, alisema ni mara ya 10 tuzo hizo kufanyika nchini na zinalenga kuhamasisha na kutoa wahitimu wenye uwezo na ubunifu ambao wataweza kubadilisha jamii zao kupitia uvumbuzi.



Mkuu wa Wilaya ya Ikungi mkoani Singida, Edward Mpogolo (kulia), akipata maelezo kutoka kwa mkulima, Juma Omari, kuhusu zao la pilipili kichaa, wakati wa maonyesho ya Nanenane katika viwanja vya Nzuguni, jijini Dodoma, jana. Wa pili kulia ni Katibu Tawala wa wilaya hiyo, Winfrida Funto. **NA MPIGAPICHA WETU**

## Samia aipongeza PASS kuinua sekta ya kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** BARIADI

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, ameipongeza asasi ya PASS kutokana na mchango wake mkubwa katika kuinua sekta ya kilimo nchini.

Samia alitoa pongezi hizo juzi mkoani Simiyu alipozindua maadhimisho ya Maonyesho ya Nanenane kitaifa, alisema kuwa asasi hiyo ni miongoni mwa taasisi zilizosaidia kwa kiwango kikubwa maendeleo ya sekta ya kilimo nchini.

PASS, ambayo ilianzishwa kwa lengo la kusaidia upatikanaji wa mikopo ya kifedha na uanzishwaji wa miradi ya kibiashara, imekuwa inasaidia wajasiriamali katika sekta ya kilimo biashara kuzifikia huduma za kifedha, ikiwa ni pamoja na kuwadhamini kupata mikopo kutoka taasisi za kifedha, hasa benki.

"Ninatambua mchango wa taasisi binafsi, ikiwamo PASS, katika kusaidia maendeleo ya kilimo nchini. Wamekuwa msaada mkubwa katika kuendeleza sekta hii muhimu ya kilimo," alisema.

"Kwa kweli ninaridhishwa na utendaji wa PASS katika kuwezesha upatikanaji wa mikopo na kusaidia maendeleo ya kilimo na uchumi wa nchi kwa ujumla, alisema Profesa Anfrew Temu, Mwenyekiti wa Bodi ya Wadhamini ya PASS.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2000, PASS imewezesha wajasiriamali takriban milioni 1.8 katika sekta ya kilimo walionufaika na mikopo inayofikia Sh. bilioni 844.9, iliyosaidia pia kutengeneza ajira kwa wananchi milioni 2.5.

Mkurugenzi Mtendaji wa PASS, Nicomed Bohay, alisema asasi yao iko mstari wa mbele katika kuunga mkono ajenda ya serikali ya kufanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda, akibainisha kuwa tayari kuna miradi 15 ya viwanda vidogo wameipatia ufadhili kupitia mikopo waliyoidhamini mwaka jana.

# Zao la migomba sasa kurasimishwa

**Na Ashton Balaigwa,** SIMUYU

TANZANIA inatarajia kurasimisha rasmi zao la migomba kwa ushirikiano kati ya Taasisi ya Kilimo Tanzania (TARI), Taasisi ya Kimataifa ya Kilimo cha Kitropiki (IITA) na Wakala wa Mbegu nchini (TOSCI), hatua ambayo inatajwa itasaidia kuleta manufaa makubwa kwa wakulima wa zao hilo.

Imeelezwa kuwa wakulima watapatiwa mbegu bora inayozaa mazao yenye tija kwa biashara.

Mratibu wa Utafiti wa zao la migomba Tanzania kutoka TARI, Kituo cha Maruku mkoani Kagera, Dk. Mpoki Shimwela, alisema hayo katika Maonyesho ya 27 ya Kilimo na Ufugaji (Nanenane) yanayoendelea katika Viwanja vya Nyakabindi mkoani Simiyu.

Dk. Shimwela alisema TARI na TOSCI mwaka huu zimeanzisha mkakati wa kuzirasimisha rasmi aina nne za mbegu kati ya 10 zilizofanyiwa utafiti, baada ya hapo aina nyingine sita zilizobaki nazo zitarasimishwa.

Zitakazorasmishwa ni NARITA 7, 18, 23 na 4, awamu itakayofuata zitarasimishwa zilizobaki, lengo ni kuhakikisha wakulima wanapata mbegu za uhakika zenye kuhimili ushindani wa magonjwa.

Alisema lengo la kufanya utafiti wa migomba ni kuongeza uzalishaji kupitia aina hizo mpya zilizofanyiwa utafiti nchini na TARI na IITA ili kuwasaidia wakulima kupata mbegu ambazo zitashindana na visumbuzi yakiwamo magonjwa.

"Migomba imekuwa ikikabiliwa na changamoto nyingi za magonjwa, wadudu, ukame na upungufu wa mbolea, lakini kwa muda mwingi kumekuwa na mbegu za kienyeji ambazo uzaaji wake umekuwa ukishuka sana kutokana na ndizi kuzaa hafifu," alisema.

Alisema tangu mwaka 2015 TARI Maruku ilianza majaribio ya mbegu mpya aina ya NARITA ambayo yalifanyika katika mikoa mitatu inayolima migomba ambayo ni Kagera, Mbeya na Kilimanjaro.

Alisema katika utafiti huo, aina 29 ziliingizwa nchini na kufanyiwa majaribio ya agrinomia, na pia waliangalia uzaaji wake, ukinzani wake na wadudu, magonjwa pamoja na kuwaita wakulima kwenye mashamba ya taasisi kuonja ndizi hizo zikilinganishwa na za kienyeji zinazolimwa kwenye maeneo husika. Alisema aina hizo zilizoitishwa ni nzuri, zinazaa zaidi, zina ukinzaji wa magonjwa, mikungu mikubwa pamoja na radha nzuri.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema mkakati wa sasa kwa kutumia watafiti kutoka taasisi hiyo ni kuondoa changamoto zinazowakabili wakulima kwa kuwaletea teknolojia za mbegu za kisasa ambazo zitaongeza tija na ufanisi ili kulima kilimo biashara, ambacho kinaendana na mahitaji ya malighafi katika uchumi wa viwanda.

Dk. Mkamilo alisema ameshatoa maelekezo kwa wakurugenzi wa vituo vyote 17 vya TARI kwa ajili kuwafuata wakulima katika maeneo yao na kuanzisha mashamba darasa ili kuwafundisha teknolojia za kisasa.

Nipashe

# TESA

Jumanne Agosti 4, 2020

TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



Ukurasa 14

**Mienendo vijana kizazi kipya inavyotia shaka**



Ukurasa 13

Teknolojia saidizi mwarobaini kuboresha elimu ya wahitaji



Ukurasa 12

**3D teknolojia itakayozalisha kitoweo mbadala maabara**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Jeshi la wadau lilivyotokomeza ukatili msimu wa karafuu Pemba





Kuokota karafuu ni kazi inayofanywa zaidi na wanawake na watoto. **PICHA MTANDAO.**

ELIMU ni ufunguo unaotokomeza changamoto kadhaa ndani ya jamii za Pemba ukiwamo udhalilishaji wanawake na watoto uliokuwa unafanywa msimo wa karafuu.

Uhamasishaji na utoaji wa elimu ya athari za unyanyasaji, umefanikisha kuiondoa jamii kwenye mazoea ya vitendo vya ukatili wa kingono dhidi ya kinamama na mabinti uliokuwa ukifanyika kwenye makambi ya kuvuna karafuu.

Ukatili huo wa kijinsia unaopewa jina la 'mali kwa mali au mpeta' unahusisha kuwanyanyasa kingono wanawake na mabinti unaofanywa na baadhi ya wanaume wanaowasaidia kupanda juu ya mikarafuu kutikisa na kuangusha karafuu nyingi na kuwarahisishia kinamama kazi ya kuziokota na kuzikusanya kwa wingi' kwa muda mfupi. Hilo linafanywa kwa makusudi kwa vile wanawake hawawezi kukwea juu ya miti na hawatapata karafuu nyingi bila mtu kupanda mtini, kutikisa matawi na kuziangusha kwa wingi.

Wanaume wanaofanya udhalilishaji huo, hukwea mitini kuzitikisa, wengine hata kuzikusanya na kuwapatia wanawake na mabinti lakini kwa sharti kuwa wanacholipwa ni ngono, huo ndiyo mpeta kwa wakazi wa Pemba, anasema Saada Salehe, mtia nia aliyetaka kugombea ubunge jimbo la Kojani wilayani Wete, lakini hakuteuliwa.

Licha ya karafuu kuwa muhimu kwa afya, ikielezwa kuwa ikitafunwa ni dawa ya maradhi ya kinywa kuanzia meno na hata koo. Huchanganywa na dawa ya meno kuimarisha afya ya fizi na sehemu ya juu au ganda la jino.

Utafiti wa tiba ya kisukari unaeleza kuwa karafuu ina dawa inayoweza kurekebisha matatizo ya kongosho na kumaliza tatizo hilo, uzuri na sifa za karafuu unaingia doa kutokana na uvunaji wake kuficha siri ya mateso na unyanyasaji wanawake.

Wanaonyanyasika ni pamoja na kinamama, wazee na mabinti wanaovuna korosho mashamba kila unapokuja msimu wa kuvuna. Na utaratibu wa unyanyasaji umepewa jina la 'mali kwa mali.'

Wanaowanyanyasa hutumia mwanya kuwa wanawake na watoto ndiyo wanaookota karafuu msituni lakini hawawezi kuzipandia juu ziliko na kuziangusha chini, anasema Saada.

Anakumbusha kuwa waathirika ni maskini wanawake, watoto , wajane, walea pweke, waliotelekezwa, wazee wanaolea wajukuu na pia wapo yatima wasio na msaada.

**MSIMU WA UVUNAJI**

Saada anasema karafuu huvunwa kwa wingi kuanzia Desemba hadi Januari na kinamama na watoto huajiriwa kama vibarua wanaookota karafuu kutoka mashamba ya wamiliki mbalimbali na hulipwa ujira wa Sh. 7,000 mpaka 8,000 kwa kila 'pishi' moja ambacho ni kipimo cha kilo tatu wanachookota na kukifikisha kwa mwenye shamba.

"Wamiliki wanaelezwa kuwa huuza kila kilo moja kwa Sh. 25,000. Kwa hiyo ni kama anawalipa Sh. 2,000 kwa kilo, licha ya kazi kubwa ya kuzifuata mashambani, kuzikusanya na kuwapelekea wamiliki."

Aidha, anasema wapo wanaoozokota karafuu kwa ajili ya kuuza wao wenyewe kiujasiriamali ili kupata pesa za kuhudumia familia zao nao wanaangukia kwenye mkumbo wa kudhalilishwa kwa vile hawawezi kupanda mitini na kuzitikisa ili kuziangusha kwa wingi.

"Kazi ya kuokota karafuu na kupata kilo moja ni ngumu fikiria kukusanya 'pishi takribani kilo tatu kuna ugumu zaidi na hapa ndipo wanaume wanapopata fursa ya kuwanyanyasa wanyonge hao. Wanafahamu kuwa wanawake na watoto hawawezi kupanda juu ya miti na kutikisa ili kuziangusha chini kwa wingi."

Wanapanda juu ya mkarafuu wenye urefu wa mita zaidi ya 10 na matawi mapana na kuwaangushia karafuu nyingi.

Lakini malipo ya kazi hiyo ni ngono bila kujali ni mzee, binti au mwanafunzi," anasema.

Wapo wengine wanaopanda na kuangusha karafuu nyingi, kuzikusanya na kuziandaa ili kila wanawake wanapofika kwenye mashamba huwapatia lakini nao wakitaka kulipwa ngono."

Mambo hayo hufanyika kwenye msimu wa karafuu unaoanzia Desemba hadi Januari kila mwaka na inafahamika kuwa chini ya mikarafuu wanawake wengi hudhalilishwa.

Hakima Ali Abdallah ni Katibu Mtendaji wa wa asasi ya Jumuiya ya Vijana Wanawake Pemba, anasema, mpeta ndicho kipindi cha kushuhudia kilio cha mimba za utoto, mabinti kurudishwa nyumbani baada ya kugundulika na ujauzito shuleni, taarifa nyingi za ubakaji na kuumiza watoto na uovu mwingi dhidi ya wanawake na watoto.

Hidaya Jabu Khamis, mjumbe wa asasi hiyo ya wanawake vijana Pemba anasema maeneo yanye visa hivyo ni pamoja na Micheweni, Chimba, Mgogoni, Shumba, Vyamboni na Wete.

Anasema, hali hiyo inatokana na kuweka makambi ya waokota karafuu na walaghai hujitosa makambini kuwanyanyasa watoto wakiwamo wenye miaka 13, 16, kinamama wakiwamo wazee na wajane.

**KUNUSURU WANAWAKE**

Mkurugenzi wa Mtendaji wa Wilaya ya Wete, Mkufu Fakhi Ali, akizungumzia mpeta anasema, ni kweli hali hiyo ilikuwapo lakini inapungua, serikali inatoa elimu kwa wananchi katika shehia zenye karafuu nyingi pamoja na waratibu wa shehia ikiwa ni pamoja na kufanya ziara katika kambi na kuzungumza na vibarua

"Hali hii inajitokeza zaidi karafuu zinapozaa kwa wingi . Hata hivyo, visa vimepungua na mwaka jana kiliripotiwa kimoja," anasema Mkufu.

Aidha, Shirika la ActionAid Tanzania, Pemba linashirikiana na jumuiya mbalimbali ikiwamo ya wanawake vijana Pemba, kuhamasisha mabadiliko kwenye jamii na kuacha vitendo hivyo.

INAENDELEA UK.12

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

# 3D teknolojia itakayozalisha kitoweo mbadala maabara

KUANZA matumizi ya teknolojia ya 3D sehemu mbalimbali duniani, kunaelezwa kuwa kumefanikisha uzalishaji nyama zinazotokana na mimea.

Lengo la kuanzisha ulaji nyama mbadala na kupunguza matumizi ya kitoweo cha mifugo hao kinacholalamikiwa kuwaua wanyama kwa wingi wasio na hatia na kuharibu mazingira kwa vile mifugo inahitaji malisho na maji mengi yote hayo yakiharibu mazingira.

Bidhaa za nyama zitokanazo na mimea zinatarajiwa kuanza kuzalishwa kwa wingi kwenye maabara na kampuni ya ‘Redefine Meat’ ya nchini Israel.

Uzalishaji huo utatanua teknolojia ya 3D kuendeleza kutunza mazingira, uhai wa wanyama na kuboresha afya.

Kwa mujibu wa Sauti ya Ujerumani -DW, kipindi cha Sayansi na Teknolojia, kampuni ya Redefine Meat iliyoko Tel-Aviv kusini mwa nchi hiyo itaanza mwishoni mwa mwaka huu kusambaza ‘nyama mimea’ sehemu nyingine nyingi.

DW inasema nyama hiyo ya maabara inaweza kutengeneza ng’ombe mzima na si sehemu tu.

“Tunaandaa nyama si vipande ni ng’ombe mzima. Tunatengeneza tishu za wanyama, damu na mafuta ili kupata minofu ya nyama mbadala.”



Nyama za maabara zinazotokana na teknolojia ya 3D hazitofautiani na kitoweo halisi cha wanyama. **PICHA :MTANDAO.**

“Mteja anaweza kuamua aina ya nyama anayotaka iwe ni steki ya kuchoma, kuandaa rosti au ya kupika kwa njia bora na kwa gharama nafuu na tunataka kufanya kazi bora zaidi,” inasema DW.

Majaribio yalikuwa yanazalisha kilo tatu hadi sita kwa saa moja lakini kwa sasa mashine zimeboreshwa na inayotarajiwa kutumiwa kuzalisha kilo zaidi ya 40 hata 100 kwa saa kwa gharama nafuu. DW inasema kuwa teknolojia ya 3D imetumiwa kuzalisha chakula kwenye maabara na kusaidia kulinda bayoanuai, kama wanyama hasa kuepusha kuchinja mifugo wasio na hatia, mazingira.

Hata hivyo si Israel pekee inayozalisha nyama ya maabara, kuna mataifa mengine yanayozalisha nyama hizo kwa kutumia teknolojia ya 3D mojawapo ni Uholanzi na nchi nyingine za Ulaya .

**3D NI NINI?**

DW inaeleza kuwa 3D ni teknolojia inayorahisisha kuwasilisha sura halisi ya kitu au taswira ya kile mtu anachokusudia kukiona na kwa kuleta muonekano halisi wa kile ambacho mhusika pengine kwenye maabara au kiwandani anakusudia kukitazama na kukijua kiuhalisia kimuundo na muonekano.

Teknolojia hiyo kwa mfano, inaleta muundo mzima na halisi wa kitu pamoja na muonekano wake kiuhalisia na katika kuzalisha nyama maabara picha za nyama halisi zinapowekwa kwenye programu za kompyuta huonekana kwa ukamilifu na uhalisia na pia huwezesha kuiga uhalisia huo kwenye kuzalisha nyama kutumia mimea.

Kwa hiyo kompyuta inazalisha nyama za mimea baada ya kuwekewa program zenye muonekano halisi wa nyama za wanyama hao kulingana na kile kinachotakiwa kama steki, minofu yenye mafuta na tishu nyinginezo kwenye minofu ya ng’ombe.

# Jeshi la wadau lilivyotokomeza ukatili msimu wa karafuu Pemba

**INATOKA UK.11**

Mratibu wa Actionaid Pemba, Severine Mapunda, anasema uhamasishaji mwaka huu ulifanyika Siku ya Wanawake Duniani kuhimiza kutokomeza udhalilishaji.

Anasema vijana wanawezeshwa kuhamasisha jamii kubadilika na pia kuondokana na muhali au desturi za kuwaonea aibu na haya wahalifu na kusababisha watuhumiwa kulindwa na kufichwa.

Akizungumzia jitihada hizo Katibu wa Jumuiya ya Vijana Wanawake Pemba, Hakima, anasema kwa kushirikiana na Actionaid wamewafikia wanawake , mabinti, wanafunzi na makundi ya wanyonge wengine kama wajane na wazee wakati wa Kampeni ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia.

Hakima anasema katika jitihada hizo wamelifikishwa suala hilo katika vyombo vya habari hasa redio na televisheni.

“Tumelifikisha na kulijadili kwenye kamati za maadili kwenye sheha. Lakini pia tumelizungumzia kwenye mikutano ya wazazi, walezi . Tunafuatilia na tuko karibu na polisi, madiwati ya jinsia polisi na idara za ustawi wa jamii na kila kesi zinapotokea tunazifikisha huko, kwa mujibu wa Hakima.

“Lakini changamoto kubwa ni muhali jumuiya tunahangaika lakini jamii zinazotendewa ukatili zinayamaliza wenyewe kwa wenyewe. Watuhumiwa na waathiriwa wanasameheana iwe ndugu au majirani wanaficha siri na kuhurumiana . Ndiyo muhali. Kuoneana aibu. Ndilo tatizo linalotusumbua. “

Anasema kuwa kuendeleza mila hizo kunakwamisha kesi mahakamani kwani hata zinapofikishwa hakuna hatua zinazoweza kuchukuliwa kwa vile waathirika hawako tayari kutoa ushahidi.

Chama cha Wanawake Wanahabari (TAMWA), Kisiwani Pemba kimekuwa bega kwa bega kufuatilia udhalilishaji kipindi cha mpeta na kwamba kinachofanyika ni kuwahi na kuzuia unyanyasaji usitokee kwa kuhamasisha jamii, kuzungumza na wanawake, mabinti na vijana wasitumie msimu huo kuwahadaa na kuwanyanyasa wanawake.

Mratibu wa TAMWA Pemba Fathia Musa Said, anasema mwaka 2019 kuanzia Januari hadi Desemba mwaka 2019 kwa wilaya ya Wete pekee matukio ya unyanyasaji kingono kama ubakaji, mimba kwa watoto yaliyoripotiwa kwao yalifikia 103 na kwamba ni kwa ujumla bila kujali msimu wa mpeta.

Anasema hata hivyo jitihada zinafanywa kutumia vyombo vya mawasiliano kama redio, televisheni na simu kutoa habari za udhalilishaji na pia kutumia mikutano ya shehia kuzungumzia masuala hayo. Suala la kuwahamasisha wananchi kujua ubaya wa udhalilishaji na kuupinga linakwenda pamoja na kuwafunza jinsi ya kutoa ushahidi na kusimamia haki zao mahakamani.

“Tunawajengea uwezo wa namna bora ya kutoa ushahidi mahakamani na huku Pemba tumewafundisha waathirika 20 namna ya kujiamini na kujibu maswali mahakamani, kujieleza na kutoa ushahidi kikamilifu. Aidha TAMWA Zanzibar imewajengea uwezo waathirika zaidi ya 40 kufahamu jinsi ya kutoa ushahidi anasema” Fathia.

“Jitihada hizi zimekuwa na mafanikio makubwa, hivi karibuni binti wa darasa la tano alipewa ujauzito , kesi ilifikishwa polisi hadi kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) lakini baba mzazi akaikwamisha ikitegemea kuwa angepewa pesa , wapatane na binti huyo afunge ndoa.”

“Kutokana na hamasa ya kujiamini na kutoa ushahidi, binti alikataa na kusaidia kufanikisha kesi kusikilizwa mahakamani. Anajitambua na anakumbusha tarehe ya kesi na yuko mstari wa mbele kushirikiana na TAMWA baada ya kujengewa uwezo , anaongeza.

**KUFUNZWA UJASIRIAMALI**

Fathia anaongeza kuwa mara nyingi udhalilishaji unachangiwa na umaskini, hivyo wanawake waathirika wamefunzwa ujasiriamali na ufugaji kuku kutengeneza sabuni, majani ya chai mbadala kwa kutumia viungo na vipodozi ili kuwainua kiuchumi.

Anasema, familia za waathirika wa unyanyasaji wamefunzwa kufuga kuku na wamepewa vifaranga 10 kila mmoja na ufugaji unafanyika kikamilifu 20 na idadi hiyo ni kwa wakazi wa Pemba na hizo zote ni jitihada za kuwaondoa wanawake kwenye umaskini na ukandamizwaji wa kingono.

Asha Abdallah Rashid, mkazi wa Kizimbani Wete ni muanthirika wa unyanyasaji akidhalilishwa na mumewe mwaka 2014, leo mambo yake yamebadilika. Ananufaika na miradi ya kijasiriamali ya TAMWA, anazalisha sabuni anazalisha vipodozi kwa kutumia mimea yenye manukato kama mikaratusi na karafuu.

“Ninatengeneza majani ya chai mbadala natumia mchaichai, karafuu, mdalasini, tangawizi. Maisha yanasonga nina uhakika wa chakula, elimu na maisha bora kwa wanangu,” anasema mama huyo na kupongeza juhudi za TAMWA.

TEKNOLOJIA
NA SABATO
KASIKA

# Teknolojia saidizi mwarobaini kuboresha elimu ya wahitaji

KATIKA kuboresha elimu kwa watu wa makundi maalum, Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, imetumia Sh. bilioni 5.9 kununulia na kusambaza vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na Teknolojia Saidizi.

Wizara inaamini kuwa teknolojia bunifu, rahisi na saidizi zinawezesha watoto wenye ulemavu kupata elimu bora zikihusisha kutumia kompyuta ndogo (mpakato) za kuweza kusoma.

Kuwapa vitimwendo vyepesi vya kuwawezesha kutembea kwa urahisi ili wawe huru shuleni na fimbo za kutembelea kwa wasioona.

Baadhi ya vitendea kazi vilivyonunuliwa na kusambazwa vinatajwa na Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Leonard Akwilapo, kuwa ni vifaa vya kuongeza usikivu kwa wahitaji wasiosikia kikamilifu.

Vifaa hivyo au shime sikio (hearing aids) kwa ajili ya wanafunzi wenye changamoto za matatizo kwenye masikio na mashine za kuandikia maandishi ya breli na fimbo nyeupe (braille kit) kwa ajili ya wasioona ni miongoni mwa vifaa vilivyonunuliwa na serikali.

Katibu Mkuu Akwilapo anasema hayo katika taarifa yake wakati akifungua Mafunzo ya TEHAMA na Teknolojia Saidizi hivi karibuni jijini Dar es Salaam na kuongeza kuwa hayo ni miongoni mwa mambo yaliyofanyika katika kipindi cha miaka minne ya serikali ya awamu ya tano.

"Mafunzo ya TEHAMA na Teknolojia Saidizi ni muhimu, kwani yamewajengea uwezo wakufunzi na walimu wa sekondari wasioona, viziwi na wenye ualbino katika matumizi ya teknolojia hiyo ili kuboresha ufundishaji, katika vyuo vya ualimu na shule za sekondari nchini," anasema Dk. Akwilapo.

Anasema, wahusika sasa wana maarifa na stadi kuhusu mfumo, vipengele na utendaji kazi wa kompyuta, utumiaji wa program saidizi za sauti na kukuza maandishi katika kompyuta.

Pamoja na hayo, anasema, sasa wanajua stadi za matumizi ya mitandao, wanapotafuta na kutuma taarifa mbalimbali kwenye tovuti na barua pepe.

Adha, wanatumia kikamilifu maudhui ya kielektroniki katika ufundishaji na ujifunzaji, anaongeza Dk. Akwilapo.

### KUBORESHA ELIMU

Mbali na ununuzi wa vifaa hivyo, anasema, katika kipindi cha miaka minne ya Rais John Magufuli, serikali imefanya upanuzi na ukarabati wa Chuo cha Ualimu Patandi mkoani Arusha, ili kuongeza udahili wa walimu kutoka 300 hadi kufikia walimu 450 kwa mwaka wa masomo 2019/2020.

Anasema, pia imejenga shule ya sekondari ya mfano katika chuo hicho yenye uwezo wa kudahili wanafunzi 640 wenye mahitaji maalumu na inasaidia wanachuo kufanya mazoezi ya kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kwa vitendo na kuwa weledi katika fani wanazosomea.

"Mnaweza kuona jitihada ambazo serikali imezifanya, hivyo nitoe wito kwa familia na wadau wa maendeleo kuendelea kuona umuhimu wa kuchangia juhudi za serikali katika kuwapatia huduma stahiki wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika ujifunzaji, " anasema.

### WITO KWA UMMA

Miongoni mwa mambo muhimu, ambayo wazazi na walezi walio na watoto wenye ulemavu, wanahimizwa ni kutowaficha ndani, badala yake watoe taarifa kwa viongozi serikali ili wapate elimu.

Wanahimizwa hivyo kutokana na ukweli kwamba, watoto walemavu nao wana haki ya kupata elimu kama walivyo wengine wenye viungo kamili, hivyo kuwaficha ni kuwakosesha haki hiyo ya msingi.

Katika hilo, Dk. Akwilapo anasema, ushiriki wa jamii ni muhimu, kwa vile masuala ya watu wenye ulemavu ni mtambuka, hivyo jitihada za pamoja zinahitajika ili kufikia malengo yaliyoainishwa katika miongozo ya kitaifa na kimataifa kwenye suala la elimu.

### WALIOFAIDI MAFUNZO

Jumla ya washiriki 140 wenye mahitaji maalum kutoka vyuo vya ualimu vya serikali na walimu wa shule za sekondari nchini, wamepata mafunzo maalum ya kuwezesha kufanya kazi yao kwa ufanisi.

Katika idadi hiyo, wasiosikia ni 37, wasioona na wenye uoni hafifu 103, huku lengo la kupewa mafunzo hayo likiwa ni kuwajengea uwezo wakufunzi na walimu katika matumizi ya TEHAMA na Teknolojia Saidizi.

Mbali na hilo, inaelezwa kuwa yanaondoa vikwazo katika vya kiutendaji lakini pia yanapunguza utegemezi na hivyo kuongeza ufanisi kwenye ufundishaji wa watu wenye mahitaji maalum.

Hiyo ni kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Elimu Maalum, wa wizara hiyo Greyson Mlanga wakati wa mafunzo hayo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya elimu kwa watu wa makundi yote.

Naye Kaimu Kamishna wa Elimu, Paulina Mkonongo anasema, mafunzo hayo ni mkakati endelevu wa serikali kuhakikisha elimu bora inatolewa kwa makundi yote, ikiwamo kuimarisha mafunzo kazini kwa kundi hili maalum.



Baadhi ya washiriki wa mafunzo ya TEHAMA na Teknolojia Saidizi kwa walimu na wakufunzi wenye mahitaji maalum wakiwa mafunzoni. **PICHA: MTANDAO**

> "Mafunzo ya Tehama na Teknolojia Saidizi ni muhimu, kwani yamewajengea uwezo wakufunzi na walimu wa sekondari wasioona, viziwi na wenye ualbino katika matumizi ya teknolojia hiyo ili kuboresha ufundishaji, katika vyuo vya ualimu na shule za sekondari nchini," anasema Dk. Akwilapo.



Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Mafunzo ya Ufundi, Dk. Leonard Akwilapo. **PICHA: MTANDAO**

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Mienendo vijana kizazi kipya inavyotia shaka

MABADILIKO kutoka kizazi kimoja hadi kingine au baada ya kupita miaka 50 kama alivyosema mwandishi nguli wa vitabu, Shaaban Robert, ni kielelezo cha jamii inakotoka na inakokwenda.

Kule inakotoka panafahamika, hupewa sifa lakini hapafuatiliwi au kutumika kama kioo, ila kupewa sifa za kupakwa mafuta kwa mgongo wa chupa, kama inavyosemwa katika Kiswahili. Mwelekeo halisi wa jamii uko katika uhuru na kila iitwapo leo vizuizi vya jadi vilivyokuwepo vinaondolewa, kuanzia kuondoa viboko shuleni hadi kufuta umuhimu wa jadi katika ndoa na malezi, kwani watu wameingia mijini, kaya ni za mchanganyiko.

Moja ya maeneo ambayo yanatoa picha ya mabadiliko ya kutoka kizazi kimoja hadi kingine au mchujo wa maadili kutoka kizazi cha uhuru hadi cha 'milenia' kinachokua sasa na kutazamiwa kuanza maisha ya familia ni burudani.

Ni eneo ambako hisia za watu zinaelezewa au kudhihirishwa kwa undani kwani watu wanazungumzia maisha ya kawaida wanavyoyoapitia tena kwa lugha inayoeleweka kwa wale wanaowasikiliza. Nyimbo za dansi, burudani kwa jumla ni kielelezo cha mazungumzo yao ya kila siku, na kwa vile nyimbo ni mazungumzo yanayochukua dakika kadhaa ni kama kipimo joto cha jamii iliyopo.



Vijana 'wakijirusha' kwenye michezo ya ngoma zinazochezwa mijini za 'kigodoro'. **PICHA: MTANDAO**

Ukisikiliza nyimbo za miziki ya wazi hasa katika miji halafu ukalinganisha na miaka ya 1960 hadi 1970 unakuta tofauti ni kubwa mno halafu kama una kumbukumbu ya nyimbo zilizosikika katika miongo tofauti unaweza kuona njia ya kupitia iliyojitokeza, bila watu kufahamu. Kwa maana hiyo nyimbo za kawaida za kufurahisha watu zinatoka katika mazingira ya kutafakari maisha ambayo vijana wanatakiwa au wanataka kuanza kuwa na familia zao wenyewe, na badala yake kuwa mivuto na mivutano ya starehe tu. Na hapa siyo suala la kukosekana watunzi wenye umahiri wa wale waliopita, ila hisia halisi zinazowazunguka kijamii, na soko la burudani wanayoyotoa hisia za awali zinafunikwa katika mivuto tu.

Wakati hali hii inajidhihirisha katika fani ya starehe au burudani, kinachoonekana pia ni kuenea kwa wale wanaoitwa watoto wanaoishi katika mazingira magumu, kulelewa katika nyumba kwa muda mfupi na kukimbia, pengine wakilalamikia mambo kadhaa. Imefika mahali makundi ya watu wanabaki barabarani bila makazi na penginepo wanapendelea maisha hayo kwani wanavuta wadau kuwapelekea misaada ya aina hii au ile kwa mfano katika barabara za katikati ya jiji la Dar es Salaam. Hapa na pale zinatokea kampeni za kuwaondoa ila wasipobadilika watarudi baada ya muda mfupi.

Ukisikiliza wimbo wenye mistari 'nimechoka kula hoteli, magenge ya mjini nimemaliza, Halima, Halima, Halima mwenzio nateseka' unapata picha ya mtu anayedharau kula njiani na kutaka kupata chakula nyumbani. Moja ya sababu za kutulia kimaadili ni kuwa vijana kwa jumla walikuwa wanamudu maisha, kwani kazi zilikuwepo za kutosha maisha. Hali hiyo ilipoanza kutetereka katika mkondo wa miaka ya 1970 na hasa ile ya 1980, maudhui nayo yakaanza kubadilika. Maudhui yalianza kuangalia tu sura na 'kuishi pamoja' kijumla, bila undani wa kinachokuja.

Unakuta mahali pa kuelezea matazamio kunakuja tu ukinzani wa utii, hali inayoonyesha udhati wa mahusiano kwa kiwango chepesi zaidi.

Jamii inawekwa pembeni ila inaibuka katika muziki wa kizazi kipya kama jamii ya mtaani na majirani wa nyumba za kupanga, siyo ndugu na jamaa.

> Mazingira hayo yanajadiliwa kitaaluma na kisiasa kama eneo maalum la kushughulikia matatizo ya 'wanawake na watoto,' ambako mtu anajiuliza kama wanaume walikuwepo watoto hao wakizaliwa, au la.

Ndipo inapoibukia taarabu ya kisasa na michapo yake, 'kwa fitina mko fiti,' ambayo angalau inagusa maisha ya kifamilia licha ya mikingamo. Nje ya hapo unakuta maudhi yaliyojaa tamaa bila mpango wa maisha, 'banjuka tu.' Licha ya kuwapo hali halisi kuwa kinachozungumzwa ni kucheza na kufurahi, Waswahili wanasema 'macho hayana pazia,' hivyo ni mlolongo wa 'ongezeko la thamani' kutokana na hali hiyo, na tunafikia hapo uwepo wa watoto wa mitaani, wanaozaliwa katika mazingira ya 'kubanjuka tu,' bila uhakika malezi.

Mazingira hayo yanajadiliwa kitaaluma na kisiasa kama eneo maalum la kushughulikia matatizo ya 'wanawake na watoto,' ambako mtu anajiuliza kama wanaume walikuwepo watoto hao wakizaliwa, au la.

Na hata kama aliyekuwepo mwanzoni hayupo tena, hakuna wengine waliojitokeza huko alikozaliwa wanaoweza kumjali kama mtoto? Unakuta jibu ni kuwa mabadiliko ya mfumo wa maisha au thamani ya kazi kiuchumi kuanzia miaka ya 80 iliondoa hali ambako mtoto anazaliwa anaingia katika uzio na kuwa mmoja wa wanafamilia, bila kubaguliwa. Jadi ilikuwa inazuia watoto kuzaliwa bila wazazi kuwa pamoja kama familia yaani mume na mke ila hata aondoke katika nyumba fulani mtoto huyo atalelewa. Baadaye, vizuizi vya kuzaa vimeondoka na malezi bora pia inavyoelekea hayapo.

Mazingira ya sasa ya maudhui ya burudani yanaonyesha kuwa hali hii inakolea zaidi badala ya kupungua pale unapotoka katika muziki wa 'kizazi kipya' cha muziki wa dansi yaani Bongo Flava uingie katika kizazi kipya cha ngoma za jadi zilizochanganyika na muziki, kwa mfano 'singeli.'

Hapo kunaongelewa kila kitu kana kwamba vijana wako katika msitu, ambako walikuwa wanaelezwa undani wa maisha na uzazi kwa siri. Ukiangalia vijana wanajikusanyia nini katika maudhui hayo unakuta labda kuna chembe ya kujiamini inayojitokeza katika wimbo huu au ule, lakini kimsingi ni mashaka matupu, kutazamia kila kitu kiharibike, kutokuamini kuwa mwenza atakuwa na dhamira njema.

## HABARI DODOMA



# Jafo amwaga chozi kuelezea adha ukosefu huduma afya

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, amejikuta akitokwa na machozi akizungumzia wanachi walivyokuwa wakipata adha na kupoteza maisha kutokana na ukosefu wa huduma za afya kwenye baadhi ya maeneo nchini.

Tukio hilo lilitokea jana alipokuwa akizungumza kuhusu mafanikio ya miaka mitano ya maboresho ya huduma ya afya ya msingi chini ya ofisi hiyo kwenye maadhimisho ya Siku ya TAMISEMI, yaliyofanyika jijini hapa.

Alisema wananchi wengi walikuwa wakipoteza maisha kutokana na kukosa huduma za afya, lakini kwa kipindi cha miaka mitano, serikali imetoa kipaumbele kwa sekta hiyo na kuondoa adha kwa wananchi.

"Kuna watu wenye uwezo hawafahamu kwamba Watanzania walikuwa wanateseka. Walikosa huduma za afya na walikuwa wanasafiri zaidi ya kilometa 140 kufuata huduma za afya, kinamama wanapata matatizo ya fistula, baada ya kupata uchungu kwa muda mrefu na vituo viko mbali," alisema.

"Watu hawafahamu kuna kinamama wangapi wamekufa kwa kukosa huduma muhimu wengine wamesafirishwa kwa baiskeli na mikokoteni," aliongeza.

**Mpaka sasa kwa awamu ya kwanza hospitali 67 zimekamilika, zikaongezwa zingine na sasa jumla ya hospitali 99 zinajengwa. Hizo za kwanza zimeanza kutoa huduma na hizo zingine zipo hatua mbalimbali ya ujenzi.**

Jafo alibainisha kuwa Watanzania wanaoishi mijini hawafahamu kama taifa limepoteza watu wengi kwa kukosa huduma.

"Leo Rais alipokuja na maono haya mapana, nimetembea nchi hii kuna watu walishakata tamaa, wako kwenye mazingira magumu sana. Fikiria mtu kwa mfano anayeishi kijiji cha Mbwera kule Kibiti, kutoka Kibiti hadi kufika kupata huduma za afya. Nenda kwa Watanzania waliokuwa wanaishi Wampembe katika Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, hadi kufika Namanyere ni watu wangapi tumewapoteza katika mazingira hayo?" Alihoji.

Waziri Jafo alisema kuna eneo linaitwa Mwilepwa hata gari na pikipiki kufika ni taabu, lakini Rais Magufuli alipotoa zaidi ya Sh. bilioni 500 na kati ya hizo zaidi ya Sh. bilioni 300 zilielekezwa kwenye ujenzi wa miundombinu.

"Rais wakati anaingia madarakani vituo vya afya vilivyokuwa vinakosekana katika maeneo mbalimbali ni vituo 115 pekee ambavyo vilikuwa vina uwezo wa kutoa huduma ya upasuaji. Rais ameamua kuwekeza ndani ya miaka mitano vituo 487 vimekamilika, hayo yote maeneo hatarishi vituo vya kisasa vimejengwa," alisema.

Pia alisema nchi tangu ilipopata uhuru hadi Rais Magufuli anaingia madarakani kulikuwa na hospitali za wilaya 77 kati ya halmashauri 185.

"Mpaka sasa kwa awamu ya kwanza hospitali 67 zimekamilika, zikaongezwa zingine na sasa jumla ya hospitali 99 zinajengwa. Hizo za kwanza zimeanza kutoa huduma na hizo zingine zipo hatua mbalimbali ya ujenzi. Tuna kila sababu ya kumshukuru Rais," alisema.

Waziri Jafo alisema pia zaidi ya zahanati 1,198 zimejengwa kwa kipindi cha miaka mitano.

Alibainisha kuwa wajawazito waliojifungua katika vituo hivyo vipya ni 219,764 na waliopata huduma ya upasuaji ni 18,826.

Awali, Mwakilishi wa Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Grace Maghembe, alisema kuna mikoa mitano ilikuwa haina kabisa hospitali za rufani za mikoa, lakini kwa sasa zimejengwa.

Aidha, alisema uboreshaji wa huduma za afya ikiwamo za kibingwa nchini umechangia kupunguza idadi ya wagonjwa kupelekwa nje ya nchi.



Washiriki wa mafunzo ya uwezeshaji wa Halmashauri ya Chemba, kuhusu utekelezaji wa kipindi cha pili cha awamu ya tatu ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), na uhakiki wa kaya za walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini wakiwa katika mafunzo ya siku tano ya kutumia vishikwambi vitakavyotumika kwenye zoezi la uhakiki, jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. **PICHA: PAUL MABEJA**

# Wataka kuanzishwa umoja wa walimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

JUMUIYA ya Wanafunzi wa Ualimu katika Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOSTA) wamekiomba Chama cha Walimu Tanzania (CWT) kuanzisha umoja wa walimu katika vyuo vingine ili kupanua wigo wa wanachama.

Ombi hilo lilitolewa jana na Katibu wa Jumuiya hiyo, Emmanuel Paschal, katika kongamano la Mwalimu Baba Lao lililofanyika katika ukumbi wa chuo hicho.

Alisema moja ya vitu ambavyo UDOSTA wanahitaji ni kuona vyuo vingi vinakuwa na umoja wa wanafunzi wanaosoma masomo ya ualimu jambo ambalo litasaidia kuongeza idadi ya wanachama.

Alisema hivi sasa UDOM kuna zaidi ya wanachama 600, hivyo wakipata na vyuo vingine nchini, CWT itakuwa kila kona ina wanachama ambao ni walimu taraji wa baadaye.

"Tunaomba CWT ilizingatie hilo lengo ni kuona kila chuo kuna umoja wa walimu. Umoja huu ni muhimu kwa sababu CWT inakuwa ikitoa ushirikiano kwa walimu tarajali jambo ambalo ni zuri kwa sababu inawaandaa kuwa walimu wanachama wa chama hicho.

Hata hivyo, alisema chama bado hakijasambaa katika vyuo vingine ambavyo vinaandaa walimu kwa ajili ya kupata wanachama.

"Pia kuna changamoto nyingine ni kukabiliwa na vyanzo vya mapato hivyo kinajiendesha kwa michango ya wanachama na wadau mbalimbali hasa CWT ndiyo imekuwa msaada mkubwa kwao," alisema.

Aidha, alisema tatizo jingine ni walimu wamekuwa wakikosa haki zao za msingi kama watumishi hasa katika suala zima la kupanda madaraja kitendo ambacho kimekuwa kikiwaumiza walimu.

"Tunaomba kutambulika kama wadau washirika wa CWT, ili kuweka mikakati maalum ya kuwapa semina mbalimbali kukitambua chama," alisema.

Alisema lengo lao ni kuona walimu wanatambulika hata wakiwa vyuoni.

# Wamiminika kujifunza kilimo bora Nanenane

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAKAZI wa mikoa ya Kanda ya Kati wametembelea maonyesho ya wakulima (Nanenane) ili kujifunza matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kilimo na mifugo kwa lengo la kukuza uchumi.

Rai hiyo ilitolewa na Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Yustina Munishi, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika banda la maonyesho la halmashauri hiyo, viwanja vya Nanenane Dodoma.

Munishi alisema Halmashauri ya Jiji la Dodoma imedhamiria kuwaonyesha Watanzania matumizi ya teknolojia mbalimbali za kuwasaidia kukuza uchumi kupitia shughuli za kilimo na kukifanya kilimo kuwa cha kibiashara na kuboresha usalama wa chakula.

"Halmashauri ya Jiji la Dodoma tumejipanga kuleta mabadiliko kupitia kilimo na kufanya kilimo kiwe kibiashara, katika eneo letu la banda la Nanenane tumeweka mfumo wa umwagiliaji maji kwa njia ya matone, ili Watanzania wajionee matumizi ya maji kidogo katika shughuli za kilimo," alisema.

"Unajua mazao ya bustani ni mazao yenye thamani kubwa sana, mfano, vitunguu, tutaonyesha teknolojia ya kuzalisha vitunguu kwa njia bora na kupata tija, ukizalisha vitunguu kwenye ekari moja unaweza pata mavuno tani 19 hata na zaidi," alisema.

Mkuu huyo alisema halmashauri inataka kuwainua wananchi kupitia kilimo cha mboga kibiashara.

"Katika banda la Jiji la Dodoma, wananchi watafundishwa kulima kibiashara chainizi, kabichi, spanishi, bilinganya, sukumawiki, karoti na mazao mengine mengi," alisema Munishi.

Alisema mazao hayo yanaonyesha jinsi mwananchi anavyoweza kukuza kipato chake.

"Tayari wananchi wa maeneo ya Ihumwa, Kikombo na Matumbulu wanazalisha mboga kwa kiwango kikubwa na kuuza nje ya Wilaya ya Dodoma, haya ni mafanikio makubwa katika dhana ya kukuza uchumi kupitia kilimo," alisema Munishi.





# JKT yawapa Nyanda za Juu mbinu za kilimo

**Na Grace Mwakalinga,** MOMBA

WAKULIMA wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini wametakiwa kulima kwa kutumia kitalu nyumba ili kutumia eneo dogo na kuzalisha kwa tija hasa mazao yanayotambaa kama vile nyanya na matango.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkuu wa Kikosi cha Jeshi la Kujenga Taifa cha (JKT) Itende, Luteni Kanali Juma Issa, wakati akizungumza na wanahabari ambao walitembelea banda hilo kwa lengo la kujifunza teknolojia mbalimbali.

Kanali Issa alisema kupitia maonyesho hayo wakulima wanahamasishwa kulima kwa kutumia kitalu nyumba teknolojia ambayo inatumia eneo dogo na kupata mazao mengi ukilinganisha na aina nyingine ya kilimo.

**Teknolojia mpya za mboga na matunda zimekuwa na msaada mkubwa katika kumsaidia mkulima kuongeza uzalishaji wa mazao yake.**

"Jeshi la Kujenga Taifa JKT, Kikosi cha Itende Mbeya tumejiandaa vyema kuwafundisha wakulima teknolojia mbalimbali za kilimo na ushauri wa kitaalamu lengo ni kuwawezesha kuongeza uzalishaji na kumnufaisha mkulima," alisema Kanali Issa.

Aidha, aliongeza kuwa JKT imekuwa na utararibu wa kutoa elimu kwa wakulima kwa kipindi cha mwaka mzima licha ya kuwa kwa kipindi hiki wamejikita zaidi kwenye maonyesho ya Nanenane.

Bwana Shamba wa JKT Itende, Kapteni Emmanuel Mwakimage, alisema katika maonyesho haya ya wakulima wamekuja na elimu mpya ya kufundisha ufugaji samaki kwa kutumia matangi teknolojia ambayo ni haina gharama na inachukua eneo dogo katika kuhudumia.

Alisema teknolojia mpya za mboga na matunda zimekuwa na msaada mkubwa katika kumsaidia mkulima kuongeza uzalishaji wa mazao yake.

Aliongeza kuwa kikosi hicho kimekuwa kikiwaandaa vijana kuwa wazalendo na kujifunza kilimo chenye tija ili kuongeza kipato lakini kujifunza kujitegemea.

Mmoja wa vijana wa kujitolea wa Jeshi la Kujenga Taifa, Jackson Yotham, alisema kupitia mafunzo hayo wamejifunza elimu ya kuzalisha mazao mbalimbali ya kilimo ikiwamo mboga na matunda.



Fundi wa zana za kilimo kutoka kampuni ya Agricom inayojihusisha na uuzaji, usambazaji wa zana hizo, Yunuc Nsekela (kushoto), akitoa maelezo kwa wananchi waliotembelea banda lake, katika maonyesho ya wakulima Nanenane kwenye viwanja vya John Mwakangale, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wajumbe kura za CCM wamiminiwa sifa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, kimewapongeza wajumbe wa Jumuiya ya Umoja wa Wazazi mkoani humo kwa kuwa watulivu na makini wakati wa upigaji wa kura za maoni za kumsaka mgombea ubunge kupitia jumuiya hiyo, ukilinganisha na chaguzi zilizopita.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Katibu wa CCM Mkoa wa Mbeya, Christopher Pallangyo, kwa kueleza kuwa jumuiya hiyo ni mfano wa kutokana na uchaguzi wake kufuata taratibu za chama na pia kwa kuwa watulivu na kudai kuwa hakuna minong'ono ya wagombea kupita kwa wajumbe wala viashiria vya rushwa.

Pallangyo alisema utaratibu wa namna ya kumpata mgombea ulikuwa wa utulivu na amani na kwamba wajumbe walizingatia kanuni na taratibu zinazotakiwa.

"Tunapongeza utaratibu wa namna wagombea walivyopatikana, hakika Jumuiya ya Wazazi mmefanya jambo jema ni mfano wa kuigwa wajumbe walitimiza wajibu wao bila viashiria vyovyote vya rushwa nawasihi wanachama tuendeleze utaratibu huu," alisema Pallangyo.

Katibu wa Siasa Itikadi na Uenezi Mkoa wa Mbeya, Bashiru Madodi, alisema mchakato wa kuwatafuta wagombea kwenye nafasi mbalimbali za uongozi kupitia kura za maoni umekamilika na kuwaomba wajumbe kuendelea kuwa na subira wakati chama kikiendelea na michakato mingine.

Madodi alisema hadi sasa hakuna mgombea ambaye amehakikishiwa nafasi yeyote ya uongozi ndani ya chama, badala yake watapatikana kupitia michakato mbalimbali ambayo itaendelea.

Katika uchaguzi wa kura za maoni kwa nafasi ya ubunge katika Jumuiya ya Wazazi Mkoa wa Mbeya watiania walikuwa wawili, ambapo wajumbe 34 kati ya wajumbe 35 walipiga kura na Bahati Ndingo akapata kura 33 na Riziki Msombe kura moja.

Lakini hivi karibuni, Pallangyo alikemea vitendo vya rushwa hasa baada ya baadhi ya watiania walioshinda kura za maoni na baadhi ya makada kushikiliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

## Sekta ya kilimo yatakiwa kufikia uchumi wa kati

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imesema sekta ya kilimo imechangia kwa kiwango kikubwa kuifikisha Tanzania kwenye uchumi wa kati unaochagizwa na maendeleo ya viwanda.

Hayo yalisemwa juzi na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Dk. Tulole Bucheyeki, alipokuwa anakagua vipando vya mazao mbalimbali vilivyopo kwenye maonyesho ya wakulima (Nanenane) Kanda ya Nyanda za Juu Kusini yanayotarajiwa kufanyika katika viwanja vya John Mwakangale jijini Mbeya.

Alisema viwanda vingi ambavyo vimeanzisha hapa nchini vinategemea malighafi zinazotokana na mazao mbalimbali ambayo mengi yanazalishwa ndani ya nchi, hivyo akasisitiza kuwa taasisi hiyo itaendelea kutoa mafunzo kwa wananchi ili waimarishe zaidi uzalishaji.

Alisema kwa sasa taasisi hiyo imegundua teknolojia zaidi ya 40 ambazo zitasaidia wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ambao utaliwezesha taifa kujitosheleza kwa chakula, malighafi za viwandani na ziada kuuzwa nje ya nchi.

Alisema mbali na teknolojia walizobuni, pia wamezalisha mbegu za mazao mbalimbali ambazo zitasambazwa kwa wananchi na kuelekezwa mbinu za kisasa za uzalishaji.

Dk. Bucheyeki alisema taasisi hiyo inawakaribisha wananchi wa maeneo mbalimbali kwenda kujifunza teknolojia za kilimo kwenye taasisi hiyo wakati wowote hata kama sio msimu wa kilimo.

Pia, alisema taasisi hiyo ina maabara ya kisasa ya kupima virutubisho mbalimbali vilivyomo kwenye udongo, ili kuwashauri wananchi kulima mazao kulingana na aina ya udongo wa kwenye mashamba yao.

Baadhi ya wananchi waliotembelea mashamba ya taasisi hiyo kwa ajili ya kujifunza, walisema mafunzo wanayoyapata yamewasaidia kuondokana na kilimo cha mazoea ambacho kilikuwa ni kwa ajili ya kujikimu kwa chakula na sasa wanazalisha kibiashara.

Mmoja wa wananchi hao, Zawadi Mzumbwe, kutoka katika Kata ya Isuto Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema awali kabla hawajaenda kujifunza kwenye taasisi hiyo walikuwa wanatumia mbegu za asili ambazo tija yake ilikuwa ndogo.

Alisema walikuwa wanapata kuanzia gunia tatu mpaka saba za mahindi kwenye ekari moja, lakini baada ya kupata mafunzo ya matumizi ya mbegu za kisasa na mbinu za kilimo bora wanapata kuanzia gunia 15 na kuendelea.





# Wazazi wahamasishwa ushirikiano na walimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZAZI na walezi wametakiwa kutoa ushirikiano kwa walimu ili kuhakikisha watoto wao wanapata elimu bora na kufaulu mitihani yao.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema hayo katika mahafali ya kwanza kwa wanafunzi waliofaulu kidato cha pili katika Shule ya Ghana, Wilaya ya Kati Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema endapo wazazi na walezi watashirikiana na walimu kutatua changamoto zinazowakabili wanafunzi, watafanikisha kwa kiasi kikubwa malengo ya walimu ya kuleta ufaulu mzuri kwa wanafunzi.

**Ni la lazima tuwe tayari kuchangia maendeleo ya shule hii ili kuondokana na mrundikano wa wanafunzi madarasani.**

Alisema kamati ya maendeleo ya elimu ya shehia ya Ghana imefanya kazi kubwa ya kuhakikisha inaanza ujenzi wa madarasa mengine mapya ili kuhamasisha wengine kuchangia ujenzi wa madarasa hayo.

Aliwataka wananchi kuchangia miradi ya kijamii ikiwamo ujenzi wa madarasa katika shule hiyo.

Alisema atahakikisha wamiliki wa viwanda vya kokoto, matofali na wachimba kifusi waliopo katika mkoa huo wanachangia malighafi hizo ili ziendeleze ujenzi wa madarasa hayo.

"Ni la lazima tuwe tayari kuchangia maendeleo ya shule hii ili kuondokana na mrundikano na wanafunzi madarasani," alisema.

Katika hatua nyingine, aliwataka wazazi na walezi kuwafichua watu wanaowapa mimba wanafunzi ili waweze kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Elimu ya shehia ya Ghana, Ali Mohammed Othman, alisema kamati imefikia katika mafanikio mazuri ikiwamo kuifanya jamii kuwa na mwamko wa masuala ya elimu, kuongeza ufaulu wa wanafunzi na kuanzisha ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Kwa upande wao wanafunzi walisema watasoma kwa bidii ili kufaulu mitihani yao na nchi kuwa na wataalamu wa fani mbalimbali.



Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC), Jaji Mkuu mstaafu Hamid Mahmoud Hamid, akizungumza na waandishi wa habari, ofisini kwake Maisara Mjini Zanzibar juzi, kuhusu maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwezi Oktoba mwaka huu. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# ZRB kuanza matumizi risiti kielektroniki

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

BODI ya Mapato Zanzibar (ZRB), imesema inakusudia kuanza kutumia mashine za kutoa risiti kwa njia ya kielektroniki (EFD) ikiwa ni sehemu ya kudhibiti upotevu wa mapato.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi, Mkurugenzi Mtendaji wa ZRB, Joseph Abdala Meza, alisema maandalizi yote ya kuanza kwa mfumo wa utoaji risiti kwa njia ya kielektroniki yamekamilika ikiwamo watendaji na maofisa wa bodi kupewa mafunzo.

Alisema mfumo wa utoaji wa risiti kwa njia ya kielektroniki unatarajiwa kuanza kufanya kazi Septemba, mwaka huu.

"Nataka kuwajulisha wananchi na wafanyabiashara kwa ujumla kwamba Bodi ya Mapato nchini (ZRB), inatarajiwa kuanza kutumia mfumo wa utoaji risiti kwa njia ya kielektroniki nchini kwa wafanyabiashara kuanzia Septemba, mwaka huu, lengo likiwa ni kudhibiti upotevu wa fedha za serikali," alisema.

Naye Ofisa Uhusiano wa ZRB, Shaaban Yahya, alisema kwa kuanzia risiti za kielektroniki zitatolewa kwa wafanyabiashara wakubwa ikiwamo wa biashara za jumla pamoja na vituo vya biashara ya mafuta.

Alisema kufuatia matumizi ya risiti za kielektroniki, bodi hiyo, inakusudia kupata Sh. bilioni 50 kwa mwaka ambazo zilikuwa zikipotea kutokana na ukosefu wa matumizi ya risiti hizo.

"Matumizi ya mashine za kielektroniki (EFD) kwa kiasi kikubwa zitasaidia kudhibiti upotevu wa fedha za mapato ambazo zilikusanywa," alisema.

Baadhi ya wafanyabiashara wamesema wanazisubiri mashine hizo za kielektroniki ambazo wanaamini kwa kiasi kikubwa zitaondoa malalamiko na usumbufu uliokuwa ukifanywa na watendaji wa taasisi hiyo.

"Mimi nimefurahishwa kwa kiasi kikubwa ujio wa mashine za EFD ambazo kwa kiasi kikubwa zitatusaidia kuondoa malalamiko yaliyokuwa yakitupata mara kwa mara kutoka kwa watendaji wa Bodi ya Mapato," alisema Ali Hamad.

# Balozi Iddi aitaka jamii kuendelea kuchukua tahadhari dhidi corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Balozi Seif Ali Iddi, amesema jamii inapaswa kuchukua tahadhari ya kuendelea kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema corona ilileta hofu, wasiwasi na simanzi dunia nzima hali iliyosababisha baadhi ya mila na taratibu za binadamu kama kupeana mikono, kuachwa kwa muda ili kuepuka maambukizi ya janga hilo.

Balozi Iddi akiwa pia ni Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda anayemaliza muda wake, alisema hayo wakati wa hafla ya kukabidhi vifaa vya kinga dhidi ya virusi vya corona kwa matumizi ya walimu na wanafunzi wa shule 12 zilizomo ndani ya jimbo hilo.

Alisema kwamba jamii kuendelea kujikinga na maambukizi ya virusi vya corona bado itakuwa ni suala la lazima katika kipindi hiki cha mpito kwa vile maradhi yanayotokana na virusi hivyo yanaendelea kuitesa dunia katika baadhi ya mataifa zikiwamo nchi za bara la Afrika.

Hata hivyo, alisema serikali ililazimika kupunguza masharti kumi yaliyoainishwa kupunguza maambukizi ya virusi hivyo baada ya jihitada kubwa iliyochukuliwa na taifa kwa kushirikiana na wananchi pamoja na taasisi za kitaifa na za kimataifa.

"Hatua za kunawa mikono kwa maji ya kutiririka, vitakasa mikono na uvaaji wa barakoa katika maeneo ya msongamano ni vyema ikaendelea kuzingatiwa na kufanywa kama suala la kawaida katika jamii," alisema.

Aliwashukuru na kuwapongeza wananchi wote kwa usikivu wao kufuata maelekezo ya serikali kuu pamoja na wataalamu wa sekta ya afya na hatimaye taifa kuendelea kubakia salama.

"Tuna mfano wa majirani wenzetu wa mataifa ya Madagascar na Botswana waliofanikiwa kudhibiti kuendelea kwa maambukizi ya virusi vya corona na kuamua kulegeza vikwazo kwa hatua kubwa ambayo sasa inawagharimu kutokana na kasi kubwa ya kurejea upya kwa maambukizi ya virusi hivyo," alisema.

Alisema ni muhimu wanafunzi na walimu kuendelea kuvitumia vifaa vya kinga kutokana na maeneo yao makubwa kuendelea kuwa na msongamano mkubwa wa watu.

Naye Katibu Tawala wa Wilaya ya Kaskazini 'B' Makame Machano Haji kwa niaba ya Mkuu wa wilaya hiyo, alimshukuru Balozi Seif kwa kukamilisha ahadi alizotoa wakati wa utumishi wake unaomalizika hivi karibuni.

Makame alisema uongozi wa wilaya hiyo tayari umeshajitolea kubeba dhima ya kuhakikisha vifaa vyote vilivyotolewa na viongozi wa serikali na jimbo kwa ajili ya kuwahudumia wananchi vinasimamiwa kwa faida na maendeleo ya wananchi wote.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## NYUMBA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL,** Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile: **Kuboresha biashara, Kulipa kodi ya nyumba, Kumalizia tenda, Kulipa ada, Kulipa matibabu n.k.**
**Mawasiliano** yetu **Dar es salaam** – 0768 928 516. **Arusha** – 0677 226 960.

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

Ndugu **FARAJA ISAYA CHUBWA** anatangaza Kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba Za usajili **MC 109 AXJ.** Kwa yeyote atakae iona Atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo Karibu kwa KUMB: **DSM/PHQ/RB/493541/2020**

115841802

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;200/2020**

**Ombi la MWANAHAMISI MATATA SALEHE,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SHABANI MOHAMED CHANDE.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 15/09/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 03/08/2020.

115841702

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.43. 2020**

**In the matter of the Estate of the late ZAKARIA SAMSON SAJILO of Mkonze within Dodoma Region**

**AND**

**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY MERABI SAMSON SAJILO**

**GENERAL CITATION**

**(RULE 75 PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 5th Day of August 2020.
Date at Dodoma this 17th Day of JUNE 2020

Presented for filling this 6TH Day of JULY 2020.

RESIDENT MAGISTRATE

115841202

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO KAWE**

**(S.M.M 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo KAWE**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 181/2020**

**Ombi la LATIFA JOHN SAMAILLA kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu BAKARI RASHIDI SAMAILLA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/08/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo ya BAKARI RASHIDI SAMAILLA.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe ..........20.......

115842102

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI NA TRELA.

**ANASTASIA FLAVIAN** MARANDU anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 126 ACC** SCANIA. Trela lenye namba za usajili **T 352 ACA.** Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi: Taarifa ya Polisi: **KIL/MOS/RB/8774/2020.**

115842602

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA TEMEKE ILIYOPO TEMEKE**

**SHAURI LA MADAI NO. 33/2020**

**JESCA VEDASTO RWEHUMBIZA**

**Dhidi ya**

**AUGUSTINO ROMANUS NJOVU**

**Kwa: AUGUSTINO NJOVU**

**KUITWA SHAURINI**

SHAURI TAJWA HAPO JUU LIMEPANGWA KUSIKILIZWA TAREHE 17/8/2020 SAA 8:30 ASUBUHI, HIVYO BASI UNATAKIWA KUFIKA HAPA MAHAKAMANI KWA TAREHE NA SAA ILIYOPANGWA HAPO JUU BILA KUKOSA WEWE MWENYEWE AU WAKILI WAKO UKIWA NA VIELELEZO VYOTE VYA KESI HII.
**ANGALIZO:** KAMA HUKUHUDHURIA SIKU ILIYOTAJWA HAPO JUU, MAHAKAMA ITAWEZA KUTOA UAMUZI/HUKUMU KUWA WEWE UMESHINDWA.
HATI HII IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA CHAPA YA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 23/7/2020.

115841402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI (S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;197/2020**

**Ombi la HALIMA BEJA MZEE,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BEJA MZEE BEJA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 04/08/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 23/07/2020.

115842001

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI.

**JULIUS KARAU KISAMBO** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 196 AGF TRUCK.** Chassis namba **100195895.** Engine namba **SL2133176.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi: Taarifa ya Polisi: **MOM/RB/588/2020.**

115841902

---

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**Sepratus K. Byarushengo** anatangaza kuungua kwa kadi ya gari aina ya Fuso yenye namba za usajili **T 263 AYB** kwenye kiwanda cha kahawa Wilayani Karagwe. Taarifa imefunguliwa kituo cha Polisi Bukoba **KAG/BUK/RB/565988/2020.**

115841102

---

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM.
MOB:
+255 - 0782253676

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# IS yaua 21 wakishambulia gereza

**KABUL,** Afghanstan

KUNDI linalojiita Dola la Kiislamu (IS) linadaiwa kuua watu 21 kwenye gereza moja la Mashariki mwa Afghanistan.

Ofisa mmoja wa eneo hilo alisema wengine 43 wamejeruhiwa katika shambulizi hilo ambalo lilitokea juzi usiku wakati mlipuaji wa kujitoa muhanga wa IS alipoligongesha gari lake lililojaa mabomu kwenye lango kuu la gereza la Jalalabad.

Ikaelezwa kuwa baada ya tukio hilo wapiganaji wakaanza kufyatua risasi dhidi ya vikosi vya usalama katika jela hiyo ya makao makuu ya mkoa wa Nangarhar, karibu kilometa 115 kutoka mji mkuu wa Afghanistan, Kabul.

**Shambulizi hilo linakuja siku moja baada ya maofisa kusema vikosi maalum vya Afghanistan vilimuua kamanda mmoja mwandamizi wa IS karibu na Jalalabad.**

Hadi kufikia jana jioni washambuliaji watatu walikuwa wameuawa lakini mapambano yaliendelea huku milio ya risasi ikisikika kutoka kwenye gereza hilo.

Msemaji wa Gavana wa Mkoa wa Nangarhar, Attaullah Khogyani, alisema waliouawa katika shambulio hilo ni pamoja na raia, wafungwa, walinzi na vikosi vya usalama vya Afghanistan.

Jeshi la Polisi la Afghanstan wanaamini wanamgambo kadhaa walikimbilia katika eneo moja la makazi na kufanya iwe vigumu kupambana nao.

Tawi la IS nchini Afghanistan linalofahamika kama IS katika Mkoa wa Khorasan, limedai kuhusika na shambulizi hilo. Makao yake makuu yako mkoani Nangarhar.

Hata hivyo, kiini cha shambulizi hilo hakijabainika haraka. Hata hivyo, baadhi ya mahabusi walitoroka wakati wa mapigano, kwa mujibu wa ofisa mmoja wa mkoa ambaye hakutaka jina lake litajwe kwa sababu hana mamlaka ya kuzungumza na wanahabari.

Gereza hilo linawahifadhi karibu wafungwa 1,500, ambao mamia kadhaa wanaaminika kuwa wanachama wa IS.

Shambulizi hilo linakuja siku moja baada ya maofisa kusema vikosi maalum vya Afghanistan vilimuua kamanda mmoja mwandamizi wa IS karibu na Jalalabad.

Msemaji wa kisiasa wa Taliban, Suhail Shaheen, aliliambia Shirika la Habari la AP kuwa kundi lake halikuhusika na shambulizi la Jalalabad.

Marekani ilifikia makubaliano ya amani na Taliban Februari. Duru ya pili na ambayo ni muhimu ya mazungumzo kati ya Taliban na uongozi wa kisiasa mjini Kabul haijaanza.

Marekani na Jumuiya ya Kujihami ya NATO wameshaanza kuwaondoa wanajeshi nchini humo kama sehemu ya masharti ya muafaka huo.

Taliban ilitangaza siku tatu za kuweka chini silaha kuanzia Ijumaa kwa ajili ya sikukuu ya Eid al-Adha. Mpango huo ulikamilika usiku wa manane juzi. **DW**



Askari wa Jeshi la Afghanistan wakiimarisha doria baada ya kutokea kwa shambulio katika gereza la Jalalabad lililoua askari 21 linalodaiwa kutekelezwa na kikundi cha IS. **PICHA: REUTERS**

## Rais aamuru uchunguzi jaribio la kuhujumu serikali

**ALGIERS,** Algeria

RAIS wa Algeria, Abdelmadjid Tebboune, ameamuru kufanyika kwa uchunguzi baada ya serikali kudai kuwapo kwa njama za mapinduzi.

Tebboune, ambaye alichaguliwa Disemba mwaka jana, amekuwa akijaribu kurejesha hali ya utulivu nchini Algeria baada ya kutokea maandamano makubwa yaliyomuondoa madarakani Abdelaziz Bouteflika.

Maofisa kadhaa waliokuwa katika serikali ya Bouteflika wamekamatwa na kufunguliwa mashtaka ya ufisadi.

Serikali ya Tebbourne inachukuwa kila hatua kuzuia kutokea maandamano kutokana na kupungua kabisa kwa mapato ya nchi kutoka kwa uuzaji wa mafuta. Wakazi wa mji mkuu wa Algiers na miji mingine ya nchi, wanakumbana na hali ngumu ya maisha, wakikosa nguvu za umeme na maji kwa siku kadhaa.

Baadhi ya benki zimeshuhudia idadi kubwa ya watu wakitoa pesa zao. Misitu kadhaa imeendelea kuteketea moto wakati huu wa msimu wa joto, jambo ambalo serikali inasema linatekelezwa makusudi.

Waziri Mkuu wa Algeria, Abdelaziz Djerad, alisema kwamba matukio ya sasa nchini humo yanastaajabisha.

Djerald alisema kwamba: "ukosefu wa maji unasababishwa makusudi, watu kadhaa wamekamatwa wakiwasha moto kwenye misitu ya nchi hiyo, huku wengine wakikamatwa wakiharibu vigingi vya umeme na kwamba matukio hayo yote yamepangwa kuvuruga utulivu wa nchi." **VOA**

## Jeshi la Israeli lakiri kuwashambulia wanamgambo

**JERUSALEM,** Israel

JESHI la Israeli limesema kuwa limezuia jaribio la uvamizi kutoka Syria na kuwauwa washukiwa wanne wa kundi la wanamgambo wanaotuhumiwa kujaribu kutega mabomu katika mpaka kati yake na Syria.

Msemaji wa Jeshi la Israeli, Luteni kanali Jonathan Conricus, alisema kuwa mapema jana, wanajeshi wa nchi hiyo walikuwa wamevamiwa kufuatia shughuli zisizokuwa za kawaida katika eneo la milima la Golan.

Conricus alisema wanajeshi hao waliwafyatulia risasi washukiwa wa wanamgambo baadhi yao wakiwa wamejihami baada ya kuwafuatilia wakitega mabomu ardhini.

Jeshi hilo lilitoa video iliyowaonesha washukiwa wanne wakikimbia kabla ya kupotea katika mlipuko uliosababishwa na shambulizi hilo.

Jeshi hilo la Israeli bado halijabainisha iwapo washukiwa hao wanne wana ushirikiano na Iran ama kundi la wanamgambo la Hezbollah ambao ni washirika wakuu wa Syria.

Hata hivyo, Conricus alisema kuwa serikali ya Israeli inailaumu serikali ya Syria kwa shambulizi hilo. Shirika la habari la serikali ya Syria, SANA, halikuthibitisha mara moja kuhusu shambulizi hilo la Israeli.

Israeli iliteka eneo hilo la milima la Golan mnamo mwaka 1967 na baadaye kulimiliki kinguvu.

Marekani ndilo Taifa la pekee linalotambua mamlaka ya Israel katika eneo hilo.

Tukio hilo linajiri huku hofu ikiongezeka katika eneo la Kaskazini la Israeli kufuatia shambulizi la angani lililosababisha kifo cha mpiganaji mmoja wa kundi la wanamgambo la Hezbollah nchini Syria.

Kufuatia shambulizi hilo, eneo la milima la Golan lilishambuliwa na mabomu kutoka Syria na Israel ikajibu kwa kushambulia maeneo ya kijeshi ya Syria na kuimarisha vikosi vyake katika eneo hilo.

Wakati huo huo, Shirika la linalofuatilia haki za binadamu nchini Syria lenye makao yake nchini Uingereza, limesema kuwa makundi ya itikadi kali na washirika wake katika eneo la Kaskazini Magharibi mwa Syria, jana yaliwaua wapiganaji 12 wa serikali ya nchi hiyo na kutibua operesheni yao. **DW**

# RONALDO ADOKEZA KUBAKIA JUVENTUS




**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo anaonekana anataka kubakia kwa angalau msimu mwingine na Juventus huku akitaka kushinda taji la tatu la Ligi Kuu ya Italia, Scudetto, na klabu hiyo.

Ronaldo alijiunga na Juve akitokea Real Madrid kwa ada ya euro milioni 100 miaka miwili iliyopita na ameonekana kuendelea kuwa kwenye kiwango chake, licha ya umri kuanza kumtupa mkono.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 35, alifunga mabao 21 kwenye Serie A msimu wa 2018-19, kabla ya msimu huu kufunga 31 wakati Juve wakishinda taji lao la tisa mfululizo la Ligi Kuu.

Miezi ya hivi karibuni kumekuwa na uvumi kwamba, Ronaldo anaweza kufikiria kuondoka kwani nyota huyo wa Ureno hajawa na mahusiano mazuri na kocha mkuu, Maurizio Sarri msimu huu.

Lakini Ronaldo ametoa ishara ya kwamba ana mipango ya kubaki klabuni hapo kwa ajili ya msimu wa 2020-21.

Aliandika kwenye ukurasa wake wa Instagram baada ya Juve kutwaa taji la Serie A Jumamosi: "Nina furaha kushinda mataji mawili mfululizo kati ya tisa yaliyopita ya Serie A na Juventus!

"Inaonekana ni rahisi, lakini si rahisi! Mwaka baada ya mwaka ni kazi ngumu inayohitaji kujitoa kweli! Sasa twende kwa taji la tatu."

Juve pia inaweza kumaliza miaka 24 ya kusubiria taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu.

Mabingwa hao mara mbili wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, kwa mara ya mwisho walitwaa taji hilo msimu wa 1995-96.

# Lukaku: Inter Milan inapita njia sahihi

**MILAN,** Italia

ROMELU Lukaku anaamini Inter Milan inapita kwenye njia sahihi baada ya kumaliza katika nafasi ya pili nyuma ya Juventus katika Ligi Kuu ya Italia, Serie A.

Ushindi wa 2-0 dhidi ya Atalanta kwenye siku ya mwisho ya ligi hiyo kulikiwezesha kikosi hicho cha kocha Antonio Conte kumaliza katika nafasi ya pili.

Lukaku alifunga mabao 23 katika mechi 36, ulikuwa ni mwanzo mzuri zaidi baada ya kujiunga na 'Nerazzurri' hao kwa euro milioni 80 akitokea Manchester United na ana matumaini mambo mazuri zaidi yanakuja.

"Serie A imemalizika, lakini bado tunajijenga na tunakwenda njia sahihi," aliandika straika huyo wa kimataifa wa Ubelgiji kwenye ukurasa wake wa Instagram.

"Asante kwa kusapoti timu kwa msimu wote huu. Kwa wachezaji wenzangu wote, mmekuwa watu wazuri. Nitajitoa sana kwa ajili yenu."

Inter ilifikisha pointi 82 ambazo pia zilifikiwa na Jose Mourinho wakati anakinoa kikosi hicho msimu wa 2009-10.

Hii ni mara ya kwanza wamepata pointi zaidi ya 79 bila kutwaa taji la Scudetto.





# *Pochettino afungua mlango kwa Barca*

**BARCELONA,** Hispania

MAURICIO Pochettino anaonekana amefungua mlango wa uwezekano wa kuinoa Barcelona baada ya kuonyesha kujutia "kuidharau" katika kauli yake aliyoitoa mwaka 2018.

Maisha ya ukocha ya Pochettino aliyatumia zaidi akiwa Tottenham, ambako alikaa miaka mitano hadi mwaka 2019, lakini Espanyol ndiko sehemu alikotengeneza jina lake na alitumia muda wake mwingi wa uchezaji akiwa kule.

Akiwa amecheza klabu mbili tu kama mchezaji, Pochettino aliiwakilisha Espanyol kwa miaka 10 na baadaye kuja kuwa kocha wa klabu hiyo mwaka 2009, miaka mitatu baada ya kutundika daluga.

Mara kwa mara ilikuwa inaripotiwa na vyombo vya habari vya Hispania kwamba, Pochettino hataweza kuinoa Barcelona ambayo ni wapinzani wakubwa wa Espanyol kutoka eneo moja la Catalunya.

Pochettino pia alionyesha kuungana na hilo mara kadhaa, lakini kauli yake ya hivi karibuni zaidi ni ile aliyoitoa mwaka 2018 wakati aliposema kamwe hataweza kuwa kocha wa Barca, Arsenal au Rosario Central kutokana kuwa na mahusiano ya karibuni zaidi na Espanyol, Spurs na Newell's Old Boys, ambapo ni timu pinzani zinazotoka sehemu moja.

Lakini sasa anaonekana kama anajutia kauli hiyo baada ya kunukuliwa majuzi na gazeti la El Pais.

"Natakiwa kuelezea jambo hilo vizuri," alisema akiliambia gazeti la El Pais.

"Nilikuwa jijini Barcelona mwaka ule na nilikutana na (Rais wa Barca, Josep Maria) Bartomeu kwenye Bar.

"Tulisalimia kwa pamoja kwa sababu tulikuwa tunawapeleka watoto katika shule moja na tulizungumza kwa dakika tano.

"Hilo likaibua uvumi kwa sababu tulikuwa na timu zinanitaka.

"Wakati waandishi waliponiuliza mimi kuhusu mkutano ule, nilitaka kuweka mambo wazi. Sikutaka kuidharau Barcelona.

"Unaweza kuzungumza mambo tofauti. Espanyol imejenga jina langu, lakini mimi si mjinga nisingeweza kutoa kauli kama ile.

"Pengine nisingeongea chochote sababu kwenye maisha hujui nini kitatokea mbeleni."

Pochettino amekuwa hana kazi tangu Novemba mwaka jana alipofukuzwa na Spurs, ikiwa ni miezi michache baada ya kuiongoza klabu hiyo kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Barca kwa sasa inanolewa na kocha Quique Setien, lakini kwa kushindwa kutetea taji la LaLiga baada ya kuchukua mikoba ya Ernesto Valverde mapema mwaka huu nafasi yake ipo shakani.

Lakini ripoti zinaeleza kwamba lazima ashinde Ligi ya Mabingwa Ulaya ili kuendelea na kibarua hicho.

HABARI MICHEZO

# BARCELONA WAACHANA NA DILI NEYMAR, MARTINEZ




**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA wamekubali hawana fedha za kumsajili Neymar au Lautaro Martinez - ikiionya kwamba inaweza kuwa kwenye matatizo hayo kwa "miaka mitatu au minne."

Hadi wakati mlipuko wa virusi vya corona unaibuka Ulaya, Barcelona walionekana kuwa na uhakika wa kumsajili straika wa Inter, Martinez.

Pia walionekana kuwa kwenye nafasi nzuri ya kumrudisha Neymar kutoka Paris Saint-Germain, miaka mitatu baada ya raia huyo wa Brazil kuondoka Camp Nou.

Lakini athari za mlipuko wa ugonjwa wa COVID-19 zinaonekana kwenye soka la dunia yote, huku ligi zikisimamishwa na kurudi zikichezwa bila mashabiki uwanjani.

Na wakati Barcelona walikuwa tayari wamefanya mazungumzo ya awali kuhusu usajili wa Martinez, mchezaji mwenzake na Lionel Messi kwenye timu ya Taifa ya Argentina, lakini sasa dili hilo linaonekana kuyeyuka.

Rais wa klabu hiyo, Josep Maria Bartomeu ameliambia gazeti la Catalunya la Sport: "Barca imezungumza na Inter kuhusu Lautaro, lakini mazungumzo yamesimama. Hali inaonyesha hatuwezi kutumia fedha nyingi kwa sasa.

"Neymar? Katika hali hii, sio jambo rahisi kwa sasa na hasa PSG wenyewe hawataki kumuuza kwa sababu ni mmoja wa wachezaji bora duniani."




# Arteta ampa sababu Aubameyang kubaki

**LONDON** England

MIKEL Arteta amempa changamoto Pierre-Emerick Aubameyang kubakia pale Arsenal na kuwa gwiji wa klabu hiyo.

Aubameyang alifunga mabao yote mawili kama alivyofanya kwenye nusu fainali dhidi ya Manchester City - wakati akiipa Arsenal ushindi wa 2-1 dhidi ya Chelsea na kubeba taji la FA, kwenye fainali iliyopigwa Uwanja wa Wembley Jumamosi.

Nyota huyo wa zamani wa Borussia Dortmund amefunga mabao 70 kwenye mashindano yote tangu alipojiunga na 'Washikabunduki' hao Januari mwaka 2018, lakini majaliwa yake yameibua uvumi mwingi.

Aubameyang mkataba wake wa sasa unamalizika mwakani, ingawa Arteta ameripotiwa mara kadhaa kuonyesha imani yake kwa mchezaji huyo wa kimataifa wa Gabon, atabaki hapo kwenye Uwanja wa Emirates.

Baada ya kuipa ushindi huo Arsenal dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja la London, Chelsea, Aubu alipewa changamoto na kocha wake kujiweka kwenye nafasi ya magwiji kama Ian Wright na Thierry Henry katika historia ya Arsenal.

"Ni jambo gumu kwenye soka, hilo kwa uhakika kabisa, na anafanya mambo kuwa rahisi angalia bao lake la pili alivyofunga," alisema Arteta.

"Mara zote tumekuwa tunapata washambuliaji bora katika klabu hii na Auba anastahili kulinganishwa na majina makubwa yaliyopita hapa. Hivyo ni wakati mzuri yeye kuendelea kubakia hapa."

# Rooney: Ferguson kocha wa kujilipua

**MANCHESTER,** England

WAYNE Rooney amebainisha kwamba, Alex Ferguson alitumia mbinu ya kujilipua wakati Manchester United ilipopoteza mara mbili kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Barcelona.

Rooney alikuwa bingwa wa Ulaya chini ya Ferguson wakati United ilipoifunga Chelsea kwa mikwaju ya penalti katika fanali ya mwaka 2008 jijini Moscow, lakini walishindwa kulitetea taji hilo msimu uliofuata kwa kufungwa na kikosi cha Pep Guardiola, Barca mjini Rome.

United ilikuwa na nafasi ya kulipiza kisasi cha kupoteza 2-0 kule kwenye mji mkuu wa Italia, wakati wa fainali ya michuano hiyo iliyopigwa dimba la Wembley mwaka 2011, licha ya Rooney kusawazisha bao la uongozi la Pedro la kipindi cha kwanza, mabao mawili kutoka kwa Lionel Messi na David Villa yakawezesha Barca kuibuka na ushindi wa 3-1.

Akizungumzia mchezo wa pili kati ya Manchester City na Real Madrid hatua ya mtoano wa timu 16, Rooney alibainisha kucheza dhidi ya timu za Hispania, inatakiwa kuwa na mbinu mbadala.

"Mara zote unakuwa kwenye wakati mgumu kucheza na timu kama Real au Barcelona kwa sababu unakwenda katika mchezo huo ukiwa huna uhakika wa kumiliki mpira," alisema Rooney.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# WILLIAN SASA NJIA NYEUPE ARSENAL

Wameshafikia muafaka baada ya kushindwana na Chelsea, kilichobaki na Gunners ni mchezaji...

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imetajwa kuongoza mbio za kumuwania winga wa Chelsea, Willian baada ya nyota huyo raia wa Brazil kushindwa kufikia makubaliano ya kusaini mkataba mpya na klabu yake hiyo.

Kwa mujibu wa gazeti la The Sun, mazungumzo baina ya wawakilishi wa Arsenal na wale wa mchezaji huo yako katika hatua za mwisho, ambapo Willian mwenye umri wa miaka 31, atajiunga nao akiwa mchezaji huru baada ya mkataba wake na Chelsea kumalizika msimu huu.

**Chelsea ilikuwa inapanga kumuongezea mkataba wa miaka mwili, lakini yeye akihitaji mkataba wa miaka mitatu jambo ambalo wameshindwa kufikia muafaka.**

Na klabu takribani tano zimetajwa kuingia katika vita ya kumuwania Willian, lakini ni Arsenal ambayo kwa mujibu wa taarifa kutoka katika vyanzo mbalimbali vya habari zinaeleza kuwa wameshafikia muafaka na kilichobaki ni mchezaji huyo kusaini mkataba wa miaka mitatu kuichezea timu hiyo ambayo ni mpinzani wa jadi wa Chelsea.

Taarifa hizo zimekolezwa zaidi na kauli ya Wakala anayemsimamia winga huyo, Kia Joorabchan ambaye amedai kuwa timu mbili kubwa zinazoshiriki Ligi Kuu ya England zimeonyesha nia ya kumsajili Willian.

"Ana ofa mbili kutoka katika timu zinazoshiriki Ligi Kuu ya England, lakini kuna ofa kutoka Ligi Kuu ya Marekani (MLS)," alinukuliwa wakala huyo.

## ZISIKUPITE

### ARSENAL YAMWANIA CARLOS

WASHINDI wa Kombe la FA, Arsenal wanawania kumsajili mlinzi wa kati wa Brazil, Diego Carlos huku Mikel Arteta akipanga marekebisho makubwa. ***(Telegraph)***

### NAPOLI KUMUACHIA KOULIBALY

RAIS wa Napoli, Aurelio De Laurentiis amesema beki wa kati wa Senegal, Kalidou Koulibaly, 28, anaweza kuruhusiwa kuhama klabu hiyo ikiwa kiwango cha thamani yake cha pauni milioni 81 kitafikiwa. ***(Sky Italia, via Metro)***

### SOLSKJAER KASI KWA SANCHO

KOCHA Ole Gunnar Solskjaer anataka Manchester United kuongeza kasi ya kumsaka mshambuliaji wa Borussia Dortmund na Uingereza, Jadon Sancho mwenye umri wa miaka 20, ili kuepuka hatua ya mvutano iliyojitokeza msimu uliopita kwa Harry Maguire. ***(ESPN)***

### AUBAMEYANG KUSAINI MITATU

ARSENAL itatoa ofa kwa mshambuliaji wake, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 31, wiki hii ya pauni milioni 250,000 kama mshahara wake wa wiki na watamuongezea miaka mitatu ya kuendelea kusalia klabuni hapo. ***(Mirror)***

### ORIGI ATAKIWA ASTON VILLA

ASTON Villa inawania kumsajili mshambulia wa Liverpool, Divock Origi mwenye umri wa miaka 25, raia wa Ubelgiji. ***(Sun)***

### MOURINHO KUMSAJILI DEENEY

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Jose Mourinho amepewa fursa ya kumsajili mshambuliaji wa Watford, Troy Deeney mwenye umri wa miaka 32, kuchukua nafasi ya Harry Kane kwa muda. ***(Mail)***

### LIVER KINARA KWA ALCANTARA

LIVERPOOL inaongoza dhidi ya Paris St-Germain katika mbio za kutaka kumsajili, Thiago Alcantara wa Bayern Munich mwenye umri wa miaka 28. ***(Mundo Deportivo, via talkSPORT)***

### UTD YAMNYATIA MAGALHAES

MTENDAJI Mkuu wa Manchester United, Ed Woodward amefanya mazungumzo na wawakilishi wa mchezaji wa Lille, Gabriel Magalhaes mwenye umri wa miaka 22, juu ya uwezekano wa uhamisho wa mlinzi huyo. ***(RMC Sport, via Express)***

### SMALLING, SKRINIAR KUPISHANA

MANCHESTER United ina matumaini ya kumtumia mlinzi Chris Smalling mwenye umri wa miaka 30, katika makubaliano ya mabadilishano na mlinzi wa Inter Milan, Milan Skriniar, mwenye umri wa miaka 25 raia wa Slovenia.

### BEN LULU MILAN, NAPOLI

AC Milan na Napoli zinafanya mazungumzo na mlinzi wa Uingereza wa timu ya Norwich City, Ben Godfrey mwenye umri wa miaka 22, baada ya timu hiyo kushuka daraja kutoka Ligi Kuu ya England. ***(Calciomercato, via Mail)***

### CARDIF YAMTAKA MOORE

KLABU ya Cardiff City inaongoza kwenye kinyang'anyiro cha kumsaka mshambuliaji wa Barnsley na Wales, Kieffer Moore, 27. ***(WalesOnline)***

## Miquissone: Bado michuano ya CAF

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya kuibebesha timu yake Kombe la FA juzi ikiwa ni siku chake wakitoka kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu msimu wa 2019-20, kiungo mshambuliaji wa Simba, Luis Miquissone amesema sasa anakwenda kujipanga kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Miquissone alisema amefurahi kutwaa zawadi ya mchezaji bora katika fainali hiyo ya Kombe la FA ambayo walikutana na Namungo FC, kwenye Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga Mjini.

"Najisikia vizuri kuona timu yangu imepata kombe lingine la FA, sina budi kumshukuru Mungu kutokana na ushindi aliotupa, sasa hivi ninajipanga kwa ajili ya msimu ujao pamoja na mashindano ya kimataifa," alisema Luis.

Alisema siri ya mafanikio yao ni kufuata kwa makini maelekezo ya mwalimu pamoja na ushirikiano uliopo kati ya wachezaji.

"Kufuata maelekezo ya kocha wetu ndio nguzo pamoja na ushirikiano tuliokuwa nao sisi wenyewe wachezaji, vile vile tunawashukuru mashabiki wetu kwa ushirikiano wao," alisema.

## Mafunzo, Uhamiaji kukiwakisha FA Zanzibar leo

**Na Hawa Abdalla,** ZANZIBAR

MICHUANO ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (ZFF) maarufu Kombe la FA, inatarajiwa kuendelea leo kwa kupigwa mchezo mmoja wa kiporo cha hatua ya 16-bora kati ya Mafunzo na Uhamiaji.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Hussein Ahmda Vuai, alisema maandalizi yote ya kuelekea michuano hiyo imekamilika ili kupata timu itakayoiwakilisha Zanzibar katika michuano ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Alisema hatua ya robo fainali ya michuano hiyo itachezwa kuanzia Agosti 10-13, huku nusu fainali ikichezwa Agosti 22, na fainali kwa upande wa Unguja itachezwa Agosti 23, mwaka huu.

Alisema kwa upande wa Kisiwa cha Pemba michuano hiyo hatua ya 16-bora itaendelea Agosti 6, mwaka huu kwa kuchezwa mchezo kati ya Chipukizi na Machomane.

"Tunaendelea na michuano ya Kombe la FA kwa mujibu wa ratiba yetu baada ya serikali kuruhusu michezo yote kuendelea, matarajio ni kuona mpaka kufikia Agosti 28, mwaka huu tayari tuwe tushapata timu itakayoiwakilisha Zanzibar katika michuano ya CAF," alisema.

# SIMBA YATOA SABABU KUTWAA UBINGWA FA

**Na Somoe Ng'itu,** RUKWA

MABINGWA wapya wa Kombe la FA, Simba ya jijini, Dar es Salaam wamesema walistahili kutwaa ubingwa wa michuano hiyo kwa sababu ya "kufaulu" kupita kwenye "njia ngumu" kuanzia hatua ya kwanza.

**Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema jana kuwa safari ya kutwaa ubingwa huo kwao ilikuwa ngumu na ubora wa kikosi chao ndio umefanikisha kuibuka washindi wa taji hilo la tatu msimu huu.**

Matola alisema walikutana na ushindani mkubwa kuanzia mechi yao ya kwanza dhidi ya Mwadui ambayo walifanikiwa kusonga mbele baada ya kuwaondoa kwa matuta.

"Halafu hatua ya robo fainali tukapangwa na Azam, mechi iliyokuwa ngumu na ya ufundi, baada ya hapo tukakutana na Yanga, Mungu ni mwema tukawapa kichapo kikubwa, na leo (juzi), hii tumeibuka mabingwa, ni kweli safari yetu ilikuwa ngumu," alisema Matola.

Aliwapongeza wachezaji wa Simba kwa kupambana na kusaka ushindi katika kila mechi waliyocheza ingawa baadhi ya michezo hawakuonyesha ubora wao kutokana na changamoto tofauti walizokutana nazo.

Aliutaja mchezo ujao wa Ngao ya Hisani dhidi ya Namungo FC hautakuwa mwepesi kwa sababu wanakutana na timu moja kwa mara ya tatu ndani ya muda mfupi.

"Tumewafunga mara mbili, naamini nao wametusoma na hawataingia uwanjani kama mechi zilizopita, tutarajie mechi nyingine bora na yenye ushindani," Matola alisema.

Aliongeza msimu ujao utakuwa na ushindani zaidi kwa sababu kila timu imejipanga kuboresha kikosi chake na kutorudia makosa waliyofanya kwenye msimu uliomalizika.

Nahodha wa Simba, John Bocco, alisema wanawashukuru mashabiki wao kwa kuwaunga mkono katika mechi zote walizocheza ingawa baadhi walipata matokeo yakuumiza.

Bocco alisema mechi zote walizocheza zilikuwa na ushindani na wachezaji walioingia uwanjani kupambana na hatimaye wamemaliza msimu kwa kuchukua makombe yote.

"Asante Mungu, tulianza kwa ubingwa na kumaliza kwa ushindi, tunaahidi msimu ujao pia tutaendelea kufanya kazi nzuri, tunawaambia mashabiki wetu tuendelee kushirikiana ili kufikia malengo, umoja na ushirikiano ni vitu muhimu katika klabu," Bocco alisema.

Simba ilitwaa Kombe la FA baada ya kuifunga Namungo mabao 2-1, shukrani magoli yaliyowekwa kimiani na Luis Miquissone na Bocco wakati bao pekee la wapinzani wao lilifungwa na Edward Manyama.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot wiki iliyopita, Eliud Ngegele (kulia), akikabidhiwa mfano wa hundi ya 13,425,330/- na Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa Tanzania, Tarimba Abbas, baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa. **PICHA: SPORTPESA**

# *Kissu anukia kumrithi Abalora Azam*

**Na Saada Akida**

WAKATI usajili ukiendelea kupamba moto, jina la kipa Mtanzania David Kissu anayekipiga Gor Mahia ya Kenya kutua mezani kwa mabosi wa Azam FC, ndiyo habari ya mjini kwa sasa.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili kutoka ndani ya uongozi wa Azam FC, ni kwamba kipa huyo anatajwa kutarajia kutua viungo vya Chamazi kuja kuchukuwa nafasi ya Razak Abalora ambaye ameachana na klabu hiyo baada ya kumaliza mkataba wake.

Chanzo chetu cha habari kimeeleza Kissu, ambaye kwa sasa yupo huru baada ya kumaliza mkataba wake na Gor Mahia, anajadiliwa na muda wowote anaweza kusaini mkataba wa kukitumikia kikosi hicho cha Mromania Aristica Cioaba.

"Kwa sasa wanataka kusajili kipa kutoka hapa nyumbani na wamemuona yule Mtanzania anayecheza Gor Mahia, hivyo jina lake lipo mezani na kuna uwezekano mkubwa wa kumsajili," kilieleza chanzo chetu.

Hata hivyo, Nipashe lilipomtafuta Kissu kuthibitisha taarifa hizo, alisema: "Na mimi nazisikia taarifa hizo kutoka kwa watu wangu wa karibu, ila hadi sasa sifahamu suala lolote kwa sababu kuna meneja anayenisimamia ndiye anajua.

"Lakini ameniambia kuna timu anafanya nazo mazungumzo, sasa hapo sijui kama wapo Azam au la, kuhusu mkataba na Gor Mahia kila kitu tumemalizana na sasa nipo huru," alisema Kissu.

Gazeti hili halikuishia hapo, likamtafuta Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', lakini alisema kwa sasa ni mapema kutaja jina la kipa gani ila wanachoangalia ni uwezekano wa kumpata kutoka hapa nchini.

"Bado hakuna mazungumzo yanayoendelea, ila tunahitaji kipa mzawa ambaye atachukua nafasi ya Razak Abarola, kuhusu ni nani, bado tunaendelea na mchakato huo," alisema Popat.

# Michezo

Jumanne Agosti 4, 2020

Nipashe




Willian njia nyeupe Arsenal

UKURASA 22

TUZO TENA...




Mkurugenzi wa Utawala na Udhibiti SportPesa, Tarimba Abbas, akimkabidhi tunzo ya Mchezaji Bora wa msimu wa kampuni hiyo, Clatous Chama (kushoto), baada ya kuwasili wakitokea mkoani Mbeya jana. Kulia ni Waziri wa Mazingira na Muungano Ofisi ya Makamu wa Rais, Mussa Azzan Zungu, ambaye alihudhuria hafla hiyo ya kuwapokea katika makao makuu ya klabu hiyo, Kariakoo jijini Dar es Salaam, akiwa ameshika mfano wa hundi ya Sh. milioni moja aliyokabidhiwa Chama kutoka SportPesa. Juzi Chama alipewa tuzo nyingine ya Mchezaji Bora wa Michuano ya FA. **PICHA: SPORTPESA**

# SIMBA YATIKISA DAR, CHAMA AKOGA NOTI

## ●●● Azielekeza kwa yatima, shangwe mwanzo mwisho uwanja wa ndege hadi Msimbazi huku tafrani...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI kikosi cha Mabingwa wa Tanzania Bara Simba, kikiwasili Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Nyerere jijini Dar es Salaam jana na kupokewa kwa mbwembwe, shangwe na baadhi ya wanachama na mashabiki wake, kiungo mshambuliaji wa timu hiyo, Mzambia Clautos Chama alikutana na tuzo nyingine sambamba na 'minoti'.

**Simba iliwasili uwanjani hapo majira ya saa 4:00 asubuhi jana, ikitokea jijini Mbeya walikolala juzi baada ya siku hiyo kutoka kuichapa Namungo FC kwa mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa katika Uwanja wa Nelson Mandela, Sumbawanga mkoani Rukwa.**

Wachezaji wa Simba, benchi la ufundi na viongozi wao baada ya kuwasili walikutana na mashabiki lukuki waliokuwa wamejitokea uwanjani hapo kuwalaki na baadaye ukaanza msafara kuelekea makao makuu ya klabu hiyo yaliyopo mtaa wa Msimbazi, Kariakoo jijini Dar es Salaam.

Baada ya kuwasili Kariakoo, Chama, alikabidhiwa hundi ya Sh. milioni moja sambamba na tuzo ya Mchezaji Bora wa Ligi Kuu Bara kutoka kwa wadhamini wakuu wa klabu hiyo, Kampuni ya SportPesa ambayo iliendesha mchakato mzima wa kusaka tuzo kwa wachezaji wao.

Hata hivyo, Chama ambaye katika mechi ya fainali ya Kombe la FA alitwaa tuzo nyingine ya Mchezaji Bora wa mashindano hayo, alisema fedha hizo zote atazitoa kwa ajili ya kusaidia yatima kwa kuwa wana mahitaji makubwa kuliko yeye ambaye kwa sasa anaendelea kupambana.

### TAFRANI

Awali ilitokea tafrani kidogo baada ya wachezaji na benchi la ufundi kuwasili na kwenda kupanda basi dogo, badala ya gari maalum la wazi lililokuwa limeandaliwa kwa ajili yao, huku baadhi ya viongozi waliopewa jukumu la kuipokea timu hiyo wakigawanyika wengine wakitaka wapande kwenye basi, wengine kwenye gari la wazi.

Hata hivyo, waliotaka wapande gari maalum wakiongozwa na mwanadada mmoja, waliweza kuwaondoa wachezaji kwenye basi na kuwapeleka kwenye gari la wazi, ambalo lilianza msafara na magari mengine kwenda klabuni kupitia Buguruni na Ilala.

Tafrani hiyo iliwashangaza baadhi ya mashabiki jambo ambalo liliwafanya kukumbushia yaliyotokea wakati timu hiyo ilipotwaa ubingwa wa Tanzania Bara, ambapo mmoja wa maofisa wa Simba ambaye ni mwanadada, alipishana na Kocha Mkuu, Sven Vandenbroeck aliyekataa wachezaji kupande gari la wazi kama alivyotaka ofisa huyo, kwa madai walikuwa kwenye maandalizi ya mechi dhidi ya Yanga.

Wachezaji wa Simba, pamoja na kushuka wakiwa na Kombe la FA, lakini walikuwa na Kombe la ubingwa wa Ligi Kuu ambayo yote walikuwa nayo kwenye gari la wazi wakishangilia pamoja na mashabiki waliojitokeza kuwalaki uwanjani na wale waliowakuta barabarani na sehemu zingine walizopita.

# Eymael afungiwa miaka miwili na faini milioni 8/-

**Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Nidhamu ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imemfungia aliyekuwa Kocha wa Yanga, Mbelgiji Luc Eymael, kwa miaka miwili kujihusisha na masuala ya soka nchini na kumtoza faini ya Sh. milioni nane kwa kosa la uchochezi na vitendo vya kibaguzi.

Hatua hiyo imetokana na maneno ya kibaguzi aliyoyatoa Eymael kwa mashabiki kabla ya Yanga kumfuta kazi Juni 27, mwaka huu ikiwa ni miezi saba tu tangu aanze kuinoa klabu hiyo.

Yanga ilisema kutokana na kauli hizo za kibaguzi uongozi umeamua kumfuta kazi Eymael kuanzia Julai 27, mwaka huu na kuhakikisha anaondoka nchini haraka iwezekanavyo.

Baadhi ya kauli hizo za Eymael ambazo alisikika akitoa, alisema: "Mashabiki hawajui mpira kazi yao ni kupiga kelele kama nyani na bata, wanafokafoka tu kama mbwa, viongozi wa klabu ni sifuri na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania lipo kwa ajili ya Simba tu".



Kupitia Ofisa Habari wa TFF, Clifford Ndimbo, alithibitisha kutolewa kwa adhabu hiyo baada ya Kamati ya Nidhamu ya shirikisho hilo kujiridhisha na alichokisema Eymael kwa kupitia video na mitandao ya kijamii.

"Ni kweli TFF imetoa adhabu hiyo na faini kwa kocha wa zamani wa Yanga, Luc Eymael, kwa maneno yake ya kibaguzi, siwezi kutoa taarifa zaidi kuhusu kifungo hicho cha miaka miwili (na faini), zungumza na mwenyekiti wa kamati ya nidhamu," alisema.

Awali, katika taarifa ya TFF baada ya Eymael kutoa kauli hizo za kibaguzi, ilieleza italifikisha suala hilo kwa Shirikisho la Soka duniani (Fifa) kwa hatua zaidi.


9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042